# UCHANGANUZI WA KISHAZI TEGEMEZI CHA KISUKUMA: MTAZAMO WA X-BAA

**LUCAS JEREMIAH**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

# UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kikubali kuipokea tasnifu hii itwayo: ñ***Uchanganuzi wa Kishazi Tegemezi cha Kisukuma: Mtazamo wa X-Baa",*** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M.A.Kiswahili - Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

é é é é é é é é é é é é é

Dr Hanna Simpassa

(Msimamizi)

é é é é é é é é é é é é .

Tarehe

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili,kutafsiri au kutoa Tasnifu hii kwa namna yoyote ile,kurudufu nakala,kurekodi bila ya idhini ya mwandishi au idhini ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi.

# TAMKO

Mimi, **Lucas Jeremiah,** nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu Kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii ya au nyingine.

é é é é é é é é é é é é é ..

Sahihi

é é é é é é é é é é é é é é .

Tarehe

# TABARUKU

Naitabaruku Tasnifu hii kwa wazazi wangu marehemu Malendeja Bupilipili, Jeremiah Bupilipili, na Tabu Luhemeja kwa kunipa malezi ya bora ya uvumilivu.

Pia ninatabaruku kwa familia yangu mke wangu Suzana Yohana, kwa kunipa ushirikiano mzuri katika maisha yangu na hasa katika masomo mungu ambariki sana.Nawambia wote ñElimu ni Ukomboziò.

## SHUKURANI

Shukrani zangu za dhati zimwendee msimamizi wangu wa utafitiwa shahada ya uzamiliya Kiswahili Dr simpassa Hanna kwa kubeba jukumu la kusimamia vyema kazi hii. Namshukru kwa ujasiri wake wa kuikosoa kazi yangu pale nilipokosea,kwa kunipa msaada wa kuendeleza nilipokwama katika kuelewa ili kufanikisha kazi hii.Naamini kuwa alivumilia vya kutosha kwa udhaifu wangu kama binadamu na kama mwanafunzi.Mafanikio ya Tasnifu hii yametokana najuhudi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha na kushauri yale yote yanayofaa kuzingatiwa katika katika utafiti huu.

Ninapenda pia kutoa kushukrani za kipekee kwa walimu wangu wote walionifundishakatia katika program ya masomo ya shahada ya uzamili ya Kiswahili ambao ni Dr Jilala, Dr Kishe, Dr Elisifa, Dr Ligembe, prof. J. S, Mdee. Mafundisho yao yameniongezea maarifa mengi kunikuza na kuniendeleza kitaaluma.

Pia nashukru wanafunzi wenzangu tuliokuwa pamoja na na kushirikiana katika masomo ya shahada ya uzamili ya Kiswahili ambao ni Mary kanichi, Said Said, N, luziga, Mungu awabariki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu na wanafunzi wote wa eneo la utafiti kwa kunipatia data za utafiti.

Kwa ujumla, Watu waliotoa michango yao ya hali na mali hadi kukamilika kazi hii ni wengi sana na ni vigumu kuwataja wote katika wasaa huu.Ila na waomba waamini kuwa michango yao imepokelewa kwa moyo mkunjufu na imesaidia kufanikisha kazi hii. Nawaomba radhi sana kwa kutowataja hapa ila mungu awajaze imani na Baraka katika maisha yao.

# IKISIRI

Uchanganuzi wa Kishazi Tegemezi Cha Kisukuma kwa mtazamo wa x-baa ni mada ambayo utafiti wake iliyofanyika kwa kushirikisha watafitiwa 98. Utafiti huu ulifanyika katika Wilaya ya Geita vijijini Mkoa wa Geita. Utafiti huu ulifanyika kwa lengo uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha kisukuma kinavyojitokeza katika lugha hiyo.Katika kukamilisha adhima hiyo tulikusanya data kwa kutumia mbinu za makitabani,hojaji na mahojiano. Mbinu zilizotumika kupata watafitiwa wa utafiti huu ni mbinu ya makusudi kutoka kwa watafitiwa 98 walioshiriki katika utafiti huu ambao wametoka shule ya Bukondo, chigunga, Nyachiluluma. Butundwe, Nyamigota, kaseme` Katoro na Lutozo Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya X-Baa ndiyo iliyotumika katika kuchanganulia vishazi tegemezi vya kisukuma.Nadharia hii husaidia kuchanganua kirai, kishazi na sentensi kwa kutekeleza majukumu haya; kubainisha miundo ya virai kwa uwazi, kueleza mahusiano ya vipashio katika kirai nomino, kuonyesha jinsi umilikaji unavyojitokeza baina ya vipashio na vingine na mwisho kuonyesha kanuni za kijumla katika kufafanua muundo wa vishazi. Kwa hiyo utafiti ufanyike zaidi katika uchanganuzi wa vishazi vya lugha nyingine za kibantu na tungo ambazo utafiti huu haukufanyika katika lugha hii ya kisukuma kwa kutumia nadharia ya x-baa.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** .......... ii

**HAKIMILIKI** .......... iii

**TAMKO** .......... iv

**TABARUKU** .......... v

**SHUKURANI** .......... vi

**IKISIRI** .......... vii

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... xi

**ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO** .......... xii

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**UTANGULIZI WA JUMLA** .......... 1

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1.2 Historia Fupi Kuhusu Nadharia ya X-BAA .......... 2

1.2.1 Historia Fupi ya Kabila la Wasukuma na Lugha Yao .......... 4

1.3 Tatizo la Utafiti .......... 4

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 5

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .......... 6

1.4.2 Malengo Mahususi .......... 6

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 7

1.7 Sababu za Kuchagua Mada .......... 7

1.8 Mawanda ya Utafiti .......... 8

1.8.1 Mipaka ya Utafiti .......... 10

1.9 Hitimisho ....................................................................................10

**SURA YA PILI ....................................................................................11**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI ....................................................................................11**

2.1 Utangulizi ....................................................................................11

2.2 Dhana ya Kishazi Tegemezi ....................................................................................11

2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Uchanganuzi wa Kishazi Tegemezi ....................................................................................17

2.4 Kiunzi cha Nadharia ya x-baa ....................................................................................20

2.5 Nadharia ya X-Baa ....................................................................................20

2.6 Hitimisho ....................................................................................26

3.1 Utangulizi ....................................................................................27

3.2 Eneo la Utafiti ....................................................................................27

3.3 Kundi Lengwa ....................................................................................27

3.4 Sampuli na Usampulishaji wa Kundi Lengwa ....................................................................................28

3.5 Maadili ya Utafiti ....................................................................................29

3.6 Mchakato wa Usampulishaji ....................................................................................29

3.6.1 Mbinu ya Usampulishaji Mpokezano ....................................................................................31

3.7 Mbinu za Kukusanyia na Kuchambulia Data ....................................................................................31

3.8 Mbinu za Kukusanyia Data ....................................................................................32

3.8.1 Hojaji ....................................................................................33

3.8.2 Mahojiano ....................................................................................34

3.9 Mbinu za Kuchanganulia Data ....................................................................................35

3.9.1 Udhati wa Mbinu za Kukusayia Data ....................................................................................37

3.10 Changamano Wakati wa Kukusanyia Data ....................................................................................37

3.11 Hitimisho ....................................................................................38

**SURA YA NNE ........................................................................................................39**

**UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ...........................................39**

4.1 Utangulizi ........................................................................................................39

4.2 Kubainisha Vishazi Tegemezi vya Kisukuma ...............................................39

4.3 Kubainisha Vishazi Tegemezi vya Kisukuma kwa Kuzingatia Kigezo cha Maana na Kimofolojia .........................................................................................41

4.3.1 Kigezo cha Maana ............................................................................................41

4.3.2 Kigezo cha Kimofolojia (Maumbo) .............................................................43

4.5 Miuundo ya Vishazi Tegemezi vya Kibantu .................................................48

4.5 Viambishi Vipatanishi, Njeo, na Yambwa/Shamirisho Vinaweza kuwa Muundo Virai Kamili .......................................................................................54

4.6 Tafsiri ya Matokeo ...........................................................................................55

4.7 Hitimisho .........................................................................................................56

**SURA YA TANO ..................................................................................................57**

**MUHUTASARI WA MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ..........57**

5.1 Utangulizi .........................................................................................................57

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .................................................................57

5.3 Mchango wa Utafiti...........................................................................................58

5.4 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Fatizi ...............................................................58

5.5 Hitimisho .........................................................................................................59

**MAREJELEO.........................................................................................................60**

**VIAMBATANISHO ..............................................................................................63**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Sampuli ya Watafitiwa ....................................................29

Jedwali Na. 4.1: Viambishi Vipatanishi, Njeo, na Yambwa /Shamirisho Vinaweza kuwa Muundo Virai Kamili ..........................................................55

## ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| N | Nomino |
| T | Kitenzi |
| W | Kiwakilishi |
| V | Kivumishi |
| E | Kielezi |
| H | Kihisishi |
| KN | Kirai Nomino |
| KT | Kirai Kitenzi |
| KV | Kirai Kivumishi |
| KE | Kirai Kielezi |
| KH | Kirai Kihusishi |
| KJ | Kijalizi |
| X | Kategoria za maneno |
| XP | Kirai Kamili cha X |
| S | Sentensi |
| KJ | Kirai Kijalizi |
| KP | Kirai Kipatanishi |
| Kn | Kirai njeo |
| Ky | Kirai yambwa |
| KB | Kirai kibainishi |
| P | Kipatanishi |
| n | njeo |
| Y | Yambwa/shamirisho |
| Kx | Kirai Kamili cha kategoria yoyote |

| | |
|---|---|
| X-BAA | Nadharia kuhusu uwakilishi wa virai |
| Sò | Sentensi kijalizi |
| XP | Kirai kamili cha X |
| KSW | Kiswahili sanifu |
| KSKM | Kisukuma |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwanzo ambayo inajaribu kutoa taarifa za awali zinazohusu Uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha kisukuma kwa kutumia nadharia X-Baa. Mtafiti ameshughulikia katika kubainisha vishazi vya kisukuma. Kuainisha vishazi hivyo kwa kuzingatia miundo yake na kuvichanganua vishazi hivyo kwa kutumia nadharia ya X-Baa. Mada ya utafiti imegawanyika sehemu nane. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusiana na mada. Aidha sehemu ya pili inabainisha tatazo la utafiti, sehemu ya tatu inaweke bayana malengo ya utafiti na sehemu tano ni maswali ya utafiti yaliyomwuongoza mtafiti kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa, sehemu ya sita ni umuhimu wa utafiti.Sehemu ya saba ni mipaka ya utafiti na sehemu ya nane ni hitimisho la sura ya kwanza.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Dhana ya kishazi tegemezi ni bebwa. Maana yake ni kishazi kilichobebwa katika muundo wa kishazi/sentensi nyingine. Kishazi bebwa ni kishazi ambacho hakiwezi kujitegemea chenyewe na ambacho kimechopekwa ndani ya kishazi kingine kikuu. Masamba (2009) anafafanua kuwa kishazi rejeshi kuwa kishazi ambacho kina uamilifu wa kurejelea kwenye kirai nomino ambacho kinakibeba. Na kishazi bebwa anafafanua kuwa ni kishazi ambacho hakiwezi kujitegemea chenyewe ambacho kimechopekwa ndani ya kishazi kingine kikiuu.Mfano wavulana *waliofaulu vizuri* watapata zawadi nono. *Waliofaulu vizuri* ni kishazi tegemezi. Kilichobebwa na kishazi kingine ambacho ni huru **watapata zawadi nono**. Sentensi hiyo iliyokibeba

kishazi tegemezi ndani yake inaitwa kishazi jumuishi. Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu uchanganuzi wa kirai,kishazi sentensi na kijalizo kwa kutumia nadharia ya X-baa. Watafiti kama kanichi (2018) aliyechunguza kirai cha kibantu kinavyoweza kuchanganuliwa, kwa kutumia nadharia ya X- baa, Koech (2013) alichunguza kijalizo cha Kiswahili kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya ya X-baa naye Olali (1997). Alitafiti kuhusu kirai cha Kiswahili kinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-baa. Watafiti wengine kama Jerono (2003), Jerom (2008), na Nyaga (2011). Watafiti hawa walitafiti vishazi huru vya Kiswahili vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X- baa. Lakini,kishazi tegemezi cha kisukuma hakijashughulikiwa katika mtazamo wa X-baa. Hivyo utafiti huu uliona ipo haja ya kuziba pengo na kupiga hatua ya kuchanganua kishazi tegemezi cha kibantu mifano kutoka katika kishazi tegemezi cha kisukuma.

## 1.2 Historia Fupi Kuhusu Nadharia ya X-BAA

Nadharia ya x-baa ni mojawapo ya nadharia pana ya utawala na ufungami ambayo hutumiwa kueleza virai na maneno katika sentensi. Katika kanuni na vigezo x-baa inabadilisha sheria za kuandika upya na kuweka zile za kanuni za kijumla. X-baa inaangazia vipengele vyote vya virai vyote na wala si vile vya aina moja pekee. Isitoshe, x-baa inaoyesha kategoria za kisintaksia zinazofungamanishwa leksimu. Nadharia hii inasisitiza kuwa kila kirai kinafuatwa masharti Fulani.Virai hivi ni lazima view tungo kiini. Nadharia hii ni ya muundo virai ambayo hufafanua mahusiano ya maneno katika kirai kimoja kupitia ujopo wake Kanuni jumuishi inasema kuwa kichwa cha kirai chochote kipewe jina la X, kwa namna ya kubainisha ujumulifu wa kanuni za muundo kirai.Kwa vile x-baa itakuwa

jina la kichwa cha kirai na pia jina la kirai kamili,X ya jina la kirai huasihiriwa kwa mlazo (ó) au (-). Kirai huwa na angalau kichwa pamoja na au bila ya viambajengo vingine (Cook na Newson:1996).

Nadharia ya x-baa iliasisiwa na Jackendoff na kuendelezwa na Chomsky katika jaribio la kuonyesha miundo ya virai vya lugha. Pamoja na nadharia hii Chomsky pia aliunda nadharia ya sarufi bia ambayo ilitumika kuchanganulia lugha mbalimbali ikijikita katika ufuataji sheria au kanuni zinazohusika katika uundaji wa maneno.Nadharia hii ilitokana na upungufu ulionekana kuwepo katika nadharia ya sarufi miundo virai. Cowper (1992), anasema kuwa kuna nadharia ya x-baa ilitolewa ili kufidia upungufu wa nadharia ya kanuni miundo virai ambayo ilihitaji kuthibitiwa.

Anaeleza kuwa nadharia ya kanuni muundo virai haikutambua uhusiano wa karibu kati ya kichwa na kijalizo chake.Anafafanua kuhusu uteuzi,yaani uwezo wa kategoria leksika kuchagua kijalizo katika tungo.Hivyo nadharia ya x-baa ilizuka kama suluhisho la upungufu huu kama asemavyo Newmeyer (1986) nadharia ya x-baa ilibadilisha kanuni za miundo virai kwa kutumia ishara hizi Xò[Kibainishi cha Xô] Xô

X ⟷ Xé

Kwa kufanya hivi kategoria zote zimekuja kuwakilishwa kwa ishara moja hivyo kuondolea mbali umuhimu wa kategoria.Aidha kinyume na nadharia ya sarufi miundo virai ambayo inaonyesha mahusiano ya ndani baina ya neno kuu na maneno mengine. Naye Haegeman (1994) anadai kuwa kulingana na nadharia hii virai vyote vinatawaliwa na neno kuu yaani X maneno hayo makuu ni vitengo vya chini kabisa hutawala maneno mengine.

### 1.2.1 Historia Fupi ya Kabila la Wasukuma na Lugha Yao

Mekacha (2011) Lugha ya Kisukuma ni lugha mojawapo ya lugha za kibantu zinazopatikana hapa Tanzania.Kisukuma ni Lugha ya kibantu inayozungumzwa nchini Tanzania na kabila la Wasukuma.Kisukuma ni lugha ambishi bainishi. Maana mzizi wa neno hubainika kwa kuongezewa viambishi awali na viambishi vifuatishi. Viambishi ambavyo huwa na dhima mbalimbali.

Wasukuma, Makaazi yao ni Mwanza, Tabora, Geita, Shinyanga, Simiyu na sehemu nyingine kama Rukwa,kigoma, nakadhalika.. Kufuatana na uainishaji wa lugha za kibantu wa Malcolm Guthrie Kisukuma kipo katika kundi la F20 na inafanana na lugha ya Kinyamwezi. Kisukuma kina lahaja zifuatazo; Lahaja ya Kinakiya (Kinyaantuzu), Kinangȏweli, Kidakama, Kinanasa, Kisumabhu, na Kinanela. Hivyo utafii huu utajikita katika Lahaja ya Kinangȏweli katika kutoa mifano yetu.Tumetumia lahaja hii kwa sababu mtafiti na watafitiwa ni wamilisi wa lahaja hiyo na hupatikana eneo kubwa la wazungumzaji wa Kisukuma katika eneo tulilofanyia utafiti.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Uchanganuzi wa vishazi tegemezi vya lugha za kibantu kwa kutumia nadharia ya X-baa ni eneo jipya katika taaluma ya sintakisia ambalo halijafanyiwa utafiti.Kutokana mapitio ya kazi tangulizi kwa kadri yalivyofafanuliwa na mtafiti yanaonyesha kazi nyingi za utafiti zilizofanywa katika sintakisia ya Kiswahili zimechunguza kirai nomino,kirai kitenzi cha kinyakyusa, kijalizo,kishazi huru arifu cha Kiswahili ni maeneo yaliyozoeleka sana.Kuna kazi chache ambazo zimegusia eneo la sentensi sharti katika lugha ya Ikigusi. Miongoni mwa kazi hizo ni katika utanzu wa sintakisia uliofanywa na Nyandago (2013) ambayo inachanganua sentensi sharti ya kigusi na

Jerono, P (2003) ambayo inachanganua kishazi huru arifu cha Kiswahili.Kwa hivyo,utafiti huu unahusu uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha kisukuma kwa mtazamo wa X-baa ni eneo ambalo bado halijafanyiwa utafiti.Kimsingi hicho ndio chanzo cha kufanya utafiti huu ili kuweza kuziba mwanya uliopo katika taaluma ya lugha.Vile vile ,Kuna mitazamo miwili tofauti ya kufafanua kishazi tegemezi ambayo ni kama ifuatavyo:

(a) (a)Mawanda mapana inayojumuisha kategoria za maneno mengine ambayo hukumushwa kama kitenzi, kiwakilishi, kielezi na kishazi tegemezi kingine.

(b) Mawanda finyu inayochukulia kishazi tegemezi kuwa na maumbo yenye O-rejeshi yanayokumusha nomino au kiwakilishi tu.

Tunaamini utafiti huu umetusaidia kueleza na kufafanua dhana hii kwa mujibu wa nadharia ya X ï Baa. Maelezo haya mawili yanatofautiana yametupa pia motisha ya kutaka kufanyia utafiti wa kina katika kishazi tegemezi.kwa sababu inawezekana kuwa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu uchanganuzi wa kishazi tegemezi katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-Baa lakini si kwa lugha ya Kisukuma.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Adamu ,(2008) anaeleza kuwa malengo ya utafiti ni yale malengo yaliyokusudiwa na mtafiti . Malengo hutueleza mtafiti anataka kupata kitu ngani mwishoni mwa utafiti wake . Keya na wenzake (1989:32) Wanasisitiza kuwa ni muhimu kudokeza kwa uwazi na umakini kile ambacho utafiti unanuia kutekeleza. Utafiti huu una malengo manne, lengo kuu na malengo mahususi.

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Jambo kubwa ambalo tumekusudia kulitimiza ni kuchunguza na kuchanganua kishazi tegemezi cha kisukuma kwa kutumia nadharia ya X-Baa ilikuona kuwa nadharia hii inajitosheleza kiuchunguzi na kuchanganulia vishazi tegemezi vya kisukuma.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ambayo yapo ndani ya lengo kuu ambayo tumekusudia kuyafanya ili kuweza kufanikisha lengo kuu ni kama ifuatavyo:

(a) Kubainisha miundo ya Vishazi tegemezi vya kisukuma kwa mujibu wa Nadharia ya x-baa.

(b) Kuchanganua vishazi tegemezi vya kisukuma kikamilifu kwa kutumia Nadharia ya x-baa.

(c) Kueleza uzuri (ufaafu) wa nadharia ya x-baa katika kuchanganulia kishazi tegemezi cha kisukuma.

(d) Kuonyesha miundo ya virai vya Kisukuma kwa kutumia wa nadharia ya X-Baa kwa kuchambua miundo ya kishazi tegemezi .

## 1.5 Maswali ya Utafiti

(i) Je, Vishazi tegemezi vya Kisukuma vina muundo upi?

(ii) Je, vishazi tegemezi vya lugha ya kisukuma vinaweza kuchnganuliwa kikamilifu kwa kutumia nadharia ya x-baa?.

(iii) Je, Nadharia ya x-baa inafaa kuchanganulia kishazi tegemezi cha lugha yaKisukuma?

(iv) Je, viambishi vipatanishi,njeo, na yambwa/shamirisho vinaweza kuwa miundo virai kamili kwa kutumia nadharia ya X-baa?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Mulokozi (2005) anasema bado tunahitaji maandishi mengi zaidi yanayotokana na utafiti wa uwaandani. Hivyo, utafiti huu una umuhimu wake kama ifuatavyo; Kwanza, utafiti huu utasaidia kukusanya data na kuzihifadhi katika maandishi.Kuna mambo mengi yamehifadhiwa vichwani mwa watu kama sehemu ya kutunza kumbukumbu utunzaji wa namna hii siyo thabiti kwani wakati wowote data hizo huweza kupotea kwa kusahaulika kutokana na maradhi au kifo.

Pili, kazi hii ina kuwa mchango wetu katika uchambuzi wa sintakisia katika lugha ya Kisukuma kwa kutumia nadharia ya X- Baa kuangalia mapengo ya utafiti na wao kuendelea na tafiti nyingine.

Tatu,ni matarajio ya mtafiti kuwa kazi hii inawafaa wanafunzi na wasomi wote wa Isimu kwa ujumla hasa watakaoshughulikia lugha za makabila(kibantu).

Nne, kuchunguza ufaafu wa nadharia ya X-Baa katika kuchanganua miundo ya vishazi tegemezi katika lugha za kibantu.

Tano, Utafiti huu umesaidia kuonyesha na kuhifadhi vishazi tegemezi vy kisukuma katika maandishi ikwa mojawapo ya lugha za kibantu.

Sita, Utafiti huu utasaidia walimu wa lugha kubaini na kutumia nadharia ya X- Baa kuchanganulia vishazi tegemezi na sentensi kwa ujumla hii ni kutokana na maarifa wanayopata katika utafiti huu.

## 1.7 Sababu za Kuchagua Mada

Sababu zilizotupa motisha kutafiti mada hii ni kutokana na Wataalamu wengi wanamitazamo tofauti kuhusu kishazi tegemezi.Wengi huchukulia kuwa kishazi

tegemezi ni sehemu ya neno au neno au kifungu cha maneno kinachotumiwa kukumsha nomino tu.Wataalamu hawa wanadai kuwa kishazi tegemezi huweza kujenga kikundi nomino na kishazi hiki huchukua dhima ya kivumishi kwa sababu kinafafanua zaidi nomino na kiwakilishi.

Mlyauka et al., (2009) wanafafanua kishazi tegemezi kuwa ni tungo yenye kitenzi kisichojikamilisha kutoa taarifa kamili .Kishazi tegemezi huhitaji kishazi huru ili kukamilisha kutoa ujumbe.Kishazi tegemezi mara nyingi huegemea kwa kubainishwa na viegama vya ï o- rejeshi katika matendo na kufanya kihitaji kukamilishwe .Tunaona kama maelezo haya ya kishazi tegemezi yanakuwa finyu na yanahitaji kupanuliwa zaidi.Jukumu la kishazi tegemezi ni kukumsha nomino na vipasho vingine zaidi katika tungo.Tunahitaji kuona iwapo maelezo haya yatafaa iwapo yanafaa basi ni aina zipi za vishazi tegemezi zinaweza kuainishwa?

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii inatokana na umuhimu wa kutumia nadharia ya kisasa yaani X-Baa katika kuchunguza vishazi tegemezi mahsusi vya lugha ya kisukuma.Pia tumechagua mada hii kwa sababu uchunguzi wetu wa awali haukuweza kupata kuona utafiti uliowahi kufanyika juu ya vishazi tegemezi vya kisukuma kwa kutumia nadharia ya X-Baa.Hivyo tukashawishika kufanyia mada hii.

## 1.8 Mawanda ya Utafiti

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI (1981:304) Upeo ni kiwango cha mwisho cha kuona au kutenda jambo.katika utafiti hatua hii inahusu uwekaji wa mipaka. Utafiti huu umejikita kuchunguza kishazi tegemezi cha Kisukuma na

hatutaingilia vishazi huru.Vishazi ambavyo vimeshughulikiwa vimehusishwa na virai vya kileksika na virai vya kiuamilifu. Utafiti huu umechambua virai ambavyo vimetumika kuunda vishazi tegemezi. Uchambuzi wa Kishazi tegemezi cha kisukuma mada yetu ya utafiti na tutachanganua mpangilio na uhusiano wake na maneno kwa kutumia X-Baa. Tumechambua miundo tofauti ya vishazi tegemezi katika sentensi kama vile kikumushi cha Kirai nomino, kikumushi cha kitenzi, kikumushi cha kitenzi jina na kikumushi cha nomino, kitenzi na kielezi.mfano madarasa yaliyokamilika haraka.

Tumepambanua pia aina tofauti za vishazi tegemezi kama vile kishazi tegemezi kivumishi na kishazi tegemezi kielezi na pia tumefafanua zaidi kishazi tegemezi kielezi kwa kutumia nadharia ya X-Baa. Tumetaja kishazi na kueleza kwa kifupi pasipo kuingia ndani isipokuwa katika kishazi tegemezi kinachounda mada yetu ya utafiti.Vishazi tegemezi huchukua muundo tofauti ya maumbo kama vile kishazi tegemezi kivumishi viwakilishi virejeshi, viunganishi tegemezi na kishazi tegemezi kielezi.

Utafiti huu umejikita katika Kisukuma .Tumetumia nadharia ya x-baa kuchunguza na kuchanganulia vishazi tegemezi ili kubaini mahusiano ya viambajengo vyake na pia mahusiano ya kishazi tegemezi na vipashio vingine katika sentensi ya Kisukuma. Utafiti huu umechambua sentensi changamano kwa sababu ina beba kishazi tegemezi ndani yake na tumejifunga kwa lugha andishi kwa sababu aghalabu huwa sahili na huweza kuchanganuliwa na pia tunachota data ya utafiti wetu lugha andishi. Fauku ya hayo utafiti huu ulihusisha wilaya ya Geita vijijini katika tarafa ya butundwe eneo ambalo mtafiti analo uzoefu.

### 1.8.1 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kubainisha miundo ya kishazi tegemezi cha kisukuma,Kuchanganua vishazi tegemezi kwa kutumia nadharia ya X-baa na pia kuonyesha miundo ya virai vya kisukuma kwa kutumia nadharia ya x-baa. Na kutumia nadharia ya X-baa kuelezea ubora wake katika kuchanganulia vishazi tegemezi vya kisukuma. Utafiti huu umefanyika Tarafa ya Butundwe, Wilayani Geita na mkoa wa Geita hususani katika shule zake za sekondari zifuatazo: Bukondo, Nyachiluluma, Butundwe, Nyamigota, Katoro, Lutozo, na Kaseme Wilayani Geita eneo ambalo mtafiti anafanyakazi na kuishi katika wilaya hiyo Geita mkoani Geita hapo.

## 1.9 Hitimisho

**K**atika sura hii vipengele kadhaa vimefafanuliwa ni kama vile utangulizi,usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Mawanda ya utafiti na mipaka,usuli wa tatizo umemsaidia mtafiti katika kuchunguza tatizo la utafiti. Na pia mtafiti ameyatumia malengo ya utafiti katika kujibu maswali ya utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii kumefanywa mapitio ya kazi tangulizi kwa nia ya kupata maarifa ya watafiti waliotangulia. Katika kuhakikisha hili, tumeanza kwa kutazama wataalamu watangulizi wanaeleza nini kuhusiana na maana ya Kishazi tegemezi mifano kutoka katika kisukuma. Kisha tukaendelea na uchambuzi wa vishazi tegemezi vya kisukuma kwa jumla. Mapitio ya kazi tangulizi yametujuza maarifa mengi kuhusu mada ya utafiti na kutuwezesha kubaini pengo la utafiti. Pia katika sura hii tumewasilisha nadharia kadhaa zilizotumika katika kuongoza uchambuzi wa data za utafiti huu.

## 2.2 Dhana ya Kishazi Tegemezi

Kishazi tegemezi ni aina ya tungo ambayo muundo wake haujitoshelezi bali huhitaji kishazi huru ili kukamilisha taarifa yake. Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha (2009) ,Inadai kuwa Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho hakiwezi kujitegemea chenyewe. Mhilu, G. G na Masebo, J. A. (2008) wanasema vishazi tegemezi ni aina ya vishazi ambavyo huwa na vitenzi visivyotoa taarifa iliyokamili.Ili vishazi hivi viweze kutoa taarifa iliyokamili, huhitaji vishazi huru kukamilisha taarifa. Mfano Msichana ***aliyechelewa jana, viongozi waliokimbia mwaka jana, Kisiki kilichokatwa……***

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2016), Wanasema kishazi tegemezi ni kishazi kinachotawaliwa na kitenzi kisaidizi ambacho muundo wake hukifanya kitegemee kitenzi cha kishazi huru ili kutoa ujumbe uliokusudiwa. Kadeghe (2006) anafafanua kuwa kishazi tegemezi ni kishazi ambacho hakitoi taarifa kamili na hujibainisha kwa

kiambishi cha maumbo ya O-rejeshi kilichomo katika kitenzi na maneno mengine yanayodokeza utegemezi.

Kadeghe (ibid) anaeleza kuwa kishazi tegemezi si lazima kikamilishwe na kishazi huru, kinaweza kukamilishwa na kishazi tegemezi .mfano, Ni**ngel**isoma ni**ngeli**faulu. Anaendelea kusema katika uainishaji wa vishazi kwa kuzingatia uwezo wa kujitegemea kunadhihilika kuwako kwa vishazi huru na vishazi tegemezi. Mambo yanayosababisha utegemezi ni haya yafuatayo:

Kwanza, Uunganishaji wa sentensi mbili kwa pamoja.

Mfano: **Mtoto amepatikana**

**mtoto amepotea**

sentensi zikiunganishwa inakuwa **mtoto *aliyepotea* amepatikana.**

**Pili,** Upachikaji wa virejeshi .mfano vyo,po,ye,o,cho ,lo,mo, ko ,po nakadhalika.

Mfano.kiti *kili**cho**letwa* kimepotea.

Maembe *yali**yo**letwa* yameoza

Tatu, Upachikaji wa viambishi vya masharti mfano **ngali, ki, ngeli**, nakadhalika.

Mfano *Angaliwahi* mapema angalimkuta hapa kabla hajaondoka.kazi yake imekuwa tofauti na waandishi wengine kwani ameonyesha kuwa kishazi tegemezi pia huweza kukamilishwa na kishazi tegemezi kiingine.Maelezo haya yametufaa sana wakati wa kubainisha sifa za kishazi tegemezi. Kiango na Khamis (2002), Wamefafanua kuwa kishazi tegemezi ni tungo ambayo haileti maana kamili ikikaa peke yake.Maana yake kamili hupatikana pale tu inapoambatanishwa kwenye kishazi huru. Kiango na Khamis (wamekwisha tajwa) wamefafanua vigezo viwili vinavyo tumika katika

kubainisha vishazi tegemezi navyo ni kwa kutumia kigezo cha maana na kigezo cha kimofolojia.

Kwa upande wa kigezo cha maana, tunaweza kutambua kama kishazi Fulani ni tegemezi kwa vile kitakuwa hakitoi maana kamili.Msomaji atabaki anajiuliza maswali kadha ambayo haya wezi kujibiwa kwa kusoma kishazi hicho. Kigezo cha pili ni kigezo cha kimofolojia.Yaani maumbo.Kuna maumbo ambayo yakijitokeza katika kishazi fulani hukifanya kishazi hicho kiwe kishazi tegemezi. Maumbo hayo mara nyingi hujitokeza mwanzoni mwa kishazi na kwenye umbo la kitenzi. Kazi yao imetusaidi sana kubaini maumbo mbalimbali ya kishazi tegemezi na dhima za kishazi tegemezi zinatumika katika uundaji wa vishazi tegemezi kwa upachikaji wa viambishi, Utumiaji wa maneno maalum kwani si kila neno linaweza kufanya kazi hiyo.

Massamba na wenzake (2001), wanasema,vishazi tegemezi ni vishazi ambavyo vikiondolewa katika muktadha wa sentensi huwa haviwezi kusimama peke yake kama sentensi zenye kuijtegemea. Hii ina maana kwamba kimuundo na kimaana vishazi hivi vimefungamana sana na vishazi vinavyoandamana navyo katika sentensi. Pia wamebainisha vishazi tegemezi kwa kutumia miundo iliyokitwa katika viambishi. Vishazi hivi vitegemezi hudhihirishwa na kuwepo kwa viambishi ndani ya muundo wake.Mfano ali**po**kuja tulifurahi., A**ki**nywa maji haya atadhurika., A**nge**lala mapema a**nge**wahikuamka.Muundo ya vishazi hivi inakitwa katika viambishi **po,nge**, na **ki.** Pia wametumia miundo iliyokitwa katika neno au maneno.Msingi wa miundo inayohusika ni **Ikiwa** nitamwona jioni nitamwelezea habari hizo**, Ili** nilale lazima nimeze vidoge. **Kama** tutaonana kesho tutapiga gumzo. Na tena wameainisha

vishazi tegemezi kwa kuzingatia miundo iliyokitwa katika udondoshaji wa kipashio mfano wa vishazi vyenye miundo ya vipashio vilivyodondoshwa ni kama ifuatavyo:

**kisukuma** **Kiswahili**

(i) **B**hatinalyo eli nulu **elo.** = Hawana hili wala **lile.**

**(ii)** Bhasumba abha bhali bhalembi (bhahwahwa) hangi **bhibi** = Hawa vijana ni waongo tena **wezi**

Kazi hii imetusaidia sana katika utafiti wetu kwani imetuonyesha taratibu za kubainisha vishazi tegemezi. Longacre (1985 :237) Aliainisha vishazi kwa mapana katika aina kuu mbili,vishazi tegemezi na vishazi viambatani.Vishazi-tegemezi ni vishazi ambavyo vikiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu haviwezi kusimama peke yake kama sentensi zenye kujitegemea. Maelezo haya yatatusaidia katika utafiti wetu hasa tutakapoanza kubainisha aina za vishazi. Obuchi na Mukhwana (2010) wameelezea viambishi katika vitenzi ambapo wametoa maelezo kwa ufupi kuhusu baadhi ya vitambulishi vya kishazi tegemezi cha Kiswahili ambavyo ni **o, lo, po, zo, vyo, cho, ki, iwapo, ingawa ngali, na ye.**

Maelezo kuhusu maumbo haya yamekuwa muhimu kwani yatatupa mwongozo wa matumizi sahihi hasa maumbo haya yametumiwa katika muktadha wa kishazi tegemezi.Aidha ufafanuzi wao kuhusu sentensi changamano utatufaa sana kuelewa muundo kishazi tegemezi.Hili linatokana na ukweli kuwa sentensi changamano ndani yake kuna kishazi tegemezi Njenge, (2013), amefafanua vishazi tegemezi ni vishazi ambavyo havijitoshelezi kimaana ili kuleta maana katika tungo vinahitaji kusaidiwa na kishazi huru. Pia ameonesha vipashio vya kishazi tegemezi kama vile ;-(i) Nomino na kitenzi kikuu. Mfano chupa iliyovunjikaé Ugonjwa *ulioibuka..*

(ii) Kiwakilishi na kitenzi.

Mfano, Huyu aliyeingiaé

Wewe unayepafahamué

Wao *watakaohitaji…*

(iii) Kiwakilishi, nomino na kitenzi mfano,Yeye kijana unayechumbiaé

Wewe mwanafunzi *usiyejitahidi…*

-Nomino, kitenzi, na kielezi .mfano madarasa yaliyokamilishwa harakaé é ., Agizo litakalotekelezwa leoé

(iv) Kitenzi jina na kitenzi mfano, Kucheka kulikosikikaé , Kucheza kusikoelewekaé é

Kazi hii imetufaa sana kwani inaonyesha bayana vipashio vya vishazi tegemezi ambavyo tutavitumia katika uchanganuzi wetu. Kingœi. (2010) Anasema vishazi tegemezi ni vishazi ambavyo hueleza hali moja inayotegemea hali nyingine kwa masharti Fulani. Mara nyingi vishazi hivi huanza kwa maneno ya masharti kama ingawa, ikiwa, endapo, iwapo, kama nakadhalika.

Waihiga (1999) anafafanua viambishi vya kurejesha hutokea kabla au baada ya mzizi wa kitenzi ili kurejelea nomino ambayo habari ya inatolewa.virejeshi huweza kutokea pia kwenye mzizi ñambaò mfano ana**ye**lia, wana**o**lindwa, viwasumbua**vyo**, amba**zo** zimepita nakadhalika. Waihiga (ibid) anaendelea kufafanua kuwa muundo wa virejeshi hutegemea ngeli. Kazi hii itatusaidia sana kuchambua virejeshi kwa kuzingatia ngeli.

Masebo (2010) anafafanua kishazi tegemezi kuwa ni kishazi kinachotawaliwa na kitenzi kisaidizi ambacho muundo wake hukifanya kutegemea kitenzi cha kishazi huru ili kuweza kutoa ujumbe uliokusudiwa. Mawazo haya tunaona yana mapungufu kwani si mara zote kishazi tegemezi hutawaliwa  na kitenzi kisaidizi tu.

Kirubi na Wengine (2007) Wanasema O-rejeshi ni kiwakilishi kinachojitokeza katika au  mwishoni wa kitenzi ambacho hurejeshwa kwa mtendaji ili kutambulisha na kumwelezea au kubainisha zaidi. O-Rejeshi hubadilikabadilika kama ni kitu hai au la na iwapo ni katika umoja ama  wingi.Ndiposa tunakuwa na ali**ye** ,wal**io**, kili**cho**, vili**vyo**, lili**lo**, zil**izo** nakadhalika.

Mdee ( 1996) anasema kishazi tegemezi ni kishazi ambacho muundo wake hukifanya kutegemea kitenzi cha kishazi huru ili kuweza kutoa ujumbe uliokusudiwa. Hali hii ya utegemezi inakinyima kishazi hiki hadhi ya kuwa sentensi.Vishazi tegemezi ambavyo hutegemea vishazi vingine katika tungo hushuka daraja na kuchukua dhima ya kikundi.Baadhi ya  vishazi huchukua dhima ya kuvumisha katika tungo ambayo kwa kawaida ni dhima ya kikundi au neno.vishazi hivi huvumisha nomino iliyokatika tungo hiyo.

Mfano.mtoto *aliyeingia* anasoma shule ya mlimani

Walimu *waliofundisha* zamani wamestsfu

Shule *iliyofunguliwa* kijijini imepata walimu

Vishazi vingine hufanya kazi ya kielezi viwapo katika tungo sawa na kikundi vielezi.mfano:

Wanafunzi watafaulu wakisoma kwa bidii

Alikimbia aliponiona

Niliwaona walipoiba mahindi.

## 2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Uchanganuzi wa Kishazi Tegemezi

Katika sehemu hii inaeleza baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu wengine waliotangulia kuhusu mada ya utafiti kishazi tegemezi cha Kibantu.Kazi hizi hutoa welekeo katika kubaini pengo la utafiti .Kwa kupitia kazi tofauti tofauti za watafiti,mtafiti ameweza kubaini pengo la utafiti kwa kudurusu kazi za watafiti wengine mfano: **N**yaga (2011) alichanganua kishazi elezi cha Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya x-baa. Alijishughulisha zaidi katika kuchunguza namna nadharia ya x-baa inavyozingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango mbalimbali. Kazi hii imetufaa kwa kuwa imetupa misingi ya nadhari ya x-baa, alisema kuwa nadharia ya x-baa huzingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti tofauti. Utafiti wake ulifanyika nchini Kenya, Nairobi.

Koech (2013), alichanganua kijalizo cha Kiswahili sanifu kwa mtazamo wa x-baa kazi hii nayo imetufaa kwa sababu ameonesha uamilifu wa kijalizo katika tungo na kubainisha miundo tofauti ya vijalizo na kudhihilisha sheria zinazotawala uunganishwaji wa vipashio vinavyojaliza virai na vishazi tegemezi katika sentensi. Pia kazi hii imetuongezea data katika utafiti wetu.utafiti huu ulifanyika nchini Kenya, Nairobi.

Mayaka (2000) alishughulikia sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano katika lugha ya Ekegusi, kazi hii itakuwa ya manufaa katika utafiti huu

kwani kishazi tegemezi ambacho tumeshughulikia ni sehemu mojawapo ya sentensi changamano.Ufafanuzi kuhusu sifa za vishazi vinaunda sentensi changamano ya Ekegusi umechangia kufafanua kishazi tegemezi cha Ekegusi.Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya,Nairobi.

Polome (1967) ameshughulikia lugha ya Kiswahili katika vitengo mbalimbali. Katika kazi hii imeshughulikia miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu tulirejelea kazi hii ili kupata Elimu pana kuhusu miundo ya sentensi za Kiswahili sanifu hasa changamano ambazo ndizo zina kishazi tegemezi.

Maw (1969) Alichunguza uhusiano wa ndani wa viambajengo katika sentensi za Kiswahili. Alishughulikia muundo wa sentensi kishazi na kategoria za makundi. Pia aligusia sentensi sharti na vishazi vyake. Hivi ni vipengele vinavyohusiana na uchanganuzi wetu wa kishazi tegemezi. Kazi hii imekuwa na manufaa kwetu kutokana na maoni tuliyochukua hasa kuhusu muundo wa sentensi na vishazi kama vijenzi vya sentensi ya Kiswahili.

Jerono, (2003) alishughulikia kishazi huru cha Kiswahili sanifu akitumia nadharia ya X-Baa kazi hii imetusaidia kwa sababu kishazi huru ndicho kinachokamilisha maana ya kishazi tegemezi.Pia ametumia nadharia X-Baa katika utafiti wake wa kishazi kiarifu. Kazi yake imetusaidia pia katika kueleza matumizi ya nadharia ya X-Baa katika uchanganuzi wa viungo vya sentensi. Anasema kuwa nadharia ya X-Baa inatumika kuelezea miundo ya virai vya kila lugha na ni miongoni mwa nadharia zinazotumika kuunda nadharia ya sarufi bia. Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya, Nairobi.

Olali (1997) kama mtafiti ametumia nadharia ya X -Baa na mchango wake umetuonyesha uhusiano wa dada katika uchanganuzi wa virai. Ameonyesha namna ya kuchanganua XP iliyo na virai vingi ndani yake.Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya Nairobi. Mbesa (2008) akinukuliwa na Koech katika utafiti wake alichanganua kishazi nomino cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa. Katika utafiti wake alifafanua vishazi vijalizi vya nomino na kitenzi na kuvichanganua kwa mtazamo wa x-baa.Kazi ya imetuongezea data za utafiti kuhusu nadharia x-baa .utafiti huu ulifanyika nchini Kenya, Nairobi.

Kanichi (2018), Yeye alijikita katika kubainisha virai nomino na kirai kitenzi vinavyojitokeza katika lugha ya Kinyakyusa kwa mtazamo wa X-baa. Utafiti wake umetusaidia kuongezea data katika utafiti wetu na utafiti huu ulifanyika nchini Tanzania. Dar-es-salaam. Matu (1991) Katika kazi yake ya ñWH- Movement in Kiswahiliò amekuwa na mchango mkubwa katika Utafiti huu Katika uchanganuzi wake ametumia nadharia ya X-Baa kama ambavyo utafiti huu umefanya. Tofauti iliyopo na utafiti huu ni kuwa yeye amejikita katika sentensi zenye maswali na vilevile kazi yake haijashughulikia miuundo ya virai vinavyounda vishazi tegemezi.

Hivyo basi inaonyesha kuwa tafiti nyingi zimefanyika kwa kutumia nadharia ya x-baa. Watafiti wengi waliotafiti walichunguza uchanganuzi wa kirai nomino, kishazi huru arifu, kishazi nomino kijalizi, kijalizi na maswali ya WH-Movement in Kiswahili katika lugha ya Kiswahili na hii imeonyesha kuwa utafiti wa uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha lugha ya Kibantu hasa kisukuma kwa kutumia nadharia ya X-Baa. Haujafanyika bado. Fauku ya hayo tafiti zilizokwishafanyika zimefanyika nchini Kenya. Kwa Tanzania utafiti wa uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha kibantu mifano

kutoka katika kisukuma kwa kutumia nadharia ya X-baa inaonyesha haujafanyika. Kutokana na matokeo ya tafiti tangulizi mtafiti ameweza kushawishika kufanya utafiti juu ya kishazi tegemezi cha kisukuma baada ya kuona kuna pengo katika tafiti hizo.

## 2.4 Kiunzi cha Nadharia ya x-baa

TUKI (2009:39) Wanasema msingi au kiunzi ni kiolezo cha mfumo wa kinadharia ambacho hutoa mwongozo wa kutumia katika uchambuzi au uchunguzi wa viwango mbalimbali vya lugha. Kadurunge (2008:387) anasema nadharia ni kanuni maalumu zinazotawala utekelezaji wa jambo Fulani. TUKI (2009), wanaeleza kuwa nadharia ni utaratibu, kanuni, na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kutekeleza jambo.

Masinjila (1992) ana maoni kuwa suala la nadharia ni muhimu sana kiasi kwamba yeyote anayejikita katika kushughulikia kazi ya kitaalam huwezi kukwepa kuzingatia nadharia. Kwani nadharia inatufanya tufikirie, tusaili, tuweke tashwishi, tuone ukweli katika ufundishaji wa isimu. Kiunzi cha nadharia ambacho kitatumika katika utafiti huu ni nadharia ya x-baa.

## 2.5 Nadharia ya X-Baa

Mwaka 1957 Chomsky alibuni nadharia ya sarufi miundo na mwaka wa 1963 akaifanyia marekebisho na kuibuka na nadharia ya sarufi zalishi geuzi maumbo. Kufikia miaka ya sabini, mabadiliko ya kafanywa na kukawa na nadharia ya wastani ambayo baadaye ilirekebishwa na kuwa nadharia ya wastani panuzi. Changamoto za kiuchanganuzi zilizojidhihirisha katika lugha kwa kutumia nadharia hizi zilipelekea

Chomsky kuibua nadharia ya umilikifu na masharti ambayo ndani yake kuna vinadharia vidogo vidogo navyo ni:

(i) X-Baa x-bar theory

(ii)Thita ï Theta theory

(iii) Utawala- Bounding theory

(iv) Umilikifu Government theory

(v)Masharti Binding theory

(vi) Uhusika case theory

Hata hivyo kuna wale wanaosema kuwa mwasisi wa nadharia ya eksibaa ni John Ross.Kuna wale wanaosema kuwa ni Jackendoff Ray (1977), Jerono (2003). Wanaisimu walioandika kuhusu nadharia ya Umilikifu na Masharti wamerejelea sana kazi ya Jackendoff ( ibid) kwa mfano Cowper(1992), Haegeman (1991), Radff (1988) .Lakini kwetu sisi mwasisi ni Chomsky (1970).Nadharia tutakayotumia katika utafiti wetu ni ile ya x-baa. Nadhari ya X-baa inayojikita katika mfumo wa muundo virai. Iliibuka ili kueleza kirai kwa ukamilifu baada ya sarufi miundo virai kushindwa kufanya hivyo. Nadharia hii huongozwa na dhana ya kichwa (neno kuu) katika kirai na uhusiano wake na vipengele vingine ambavyo vimetumika kuunda kirai hicho.

Dhana ya X-baa ilingizwa katika uchanganuzi wa sentensi ilikuwezesha ujumlishaji wa sifa zinazojitokeza katika aina mbalimbali za virai kama vile kirai nomino,kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kielezi na kirai kihusishi. Sarufi miundo Virai iliyopendekezwa badala ya ile ya sarufi miundo virai. Hoja ya msingi katika nadharia hii ni kwamba sheria za sarufi miundo virai hazina budi kudhibitiwa na kwamba kategoria zaidi za virai hazina budi kuongezwa.kwa mfano katika kategoria ya KN

(kirai nomino) kuna haja ya kuingiza kategoria nyingine ambazo ni kubwa kuliko nomino lakini ndogo kuliko kirai.Alama (x) husimamia kichwa (neno kuu) katika kirai na alama ya kistari (- ) au ritifa (ó ) au baa husimamia vipashio vinavyofuatana na neno kuu (x ) katika kirai husika.

Nadharia ya x-baa ilitangulizwa na Chomsky (1970) na inashughulikia jaribio la awali kabisa la kupata suluhisho la tatizo la sarufi miundo virai. Haegeman (1994; 105) Anadai kuwa kulingana na nadharia hii virai vyote vinavyotawaliwa na neno kuu.ufasiri wa neno kuu la kirai ni sifuri. Radford (1988) ameeleza kuhusu nadharia ya X-baa. Anasema kuwa nadharia ya X-baa inazingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi.Ni upangaji unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki. Tumechagua nadharia hii kwa sababu inashughulikia jaribio la awali kabisa la kupata suluhisho la tatizo la sarufi miundo virai kuwa na sheria nyingi mno .Pili nadharia hii inaruhusu kategoria zaidi za virai kuongezwa mfano katika.

Kategoria ya virai nomino kunahaja ya kuongeza kategoria nyingine ambayo ni kubwa kuliko nomino lakini ndogo kuliko kirai (Massamba 2004) .Tatu nadharia ya x-baa inafidia upungufu wa nadharia ya kanuni miundo virai ambayo ilihitaji kuthbitiwa .Nne nadharia ya x-baa inazingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi Mwisho nadharia hii hutumika katika kuonesha na kusawazisha miundo ya virai.Pia nadharia hii inatofautisha viwango viwili vingine vya ufasiri wa ñbarò moja yaani ñxò.Pia tumeichagua ili kuona kama inafaa kuonyesha na kusawazisha muundo ya vishazi.

Cowper (1992) anasema kuwa nadharia ya x-baa ilitolewa ili kufidia upungufu wa nadharia ya kanuni miundo virai ambayo ilihitaji kuthibitiwa .Anaeleza kuwa nadharia ya kanuni miundo virai haikutambua uhusiano wa karibu kati ya kichwa na kijalizo chake .anafafanua kuhusu uteuzi, yaani uwezo wa kategoria kileksika kuchagua kijalizo katika tungo.

Radford (2004) anaeleza kuhusu uwili wa nadharia ya x-baa .Anasema kuwa kifundo hugawika katika matawi mawili pekee hivi ni kusema kuwa kirai nomino (KN) hakiwezi kuzalisha matawi matatu .Maelezo yake ni muhimu kwetu kwa sababu tutatumia kielelezo cha matawi kuchanganua kishazi kitegemezi.

Haegeman (1991) katika kuelezea nadharia ya x-baa ameeleza kuhusu uchanganuzi wa virai kwa kuzingatia kategoria na vile vile uchanganuzi wa vishazi. Anasema kuwa katika nadharia ya x-baa kirai humilikiwa kichwa lekisika. Nadharia hii inadai kwamba katika lugha zote kirai huwa na kichwa lakini mpangilio wa vipashio vinavyofuata kichwa hicho hutegemea lugha binafsi. Kwa mfano katika kirai nomino ñmtoto wanguò kichwa ni nomino ñmtotoò ilhali katika kirai kitenzi ñanacheza vizuriò kichwa ni kitenzi ñanachezaò. Kutokana na maelezo hapo juu tunapata kuwa nadharia ya X-baa ina mihimili ifuatayo:

**(i) Kila kirai huwa na neno kuu**

Neno kuu katika kirai cha kibantu au Kiswahili, huwa ni neno la kwanza. Katika kirai nomino, neno kuu ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Kwa mfano katika sentensi: Mwanafunzi mkorofi alimpiga mwalimu. Kichwa (neno kuu) cha kirai nomino ni ñMwanafunziò

**(ii) Vipashio katika kirai hupangwa katika ngazi tofauti**

Hadhi ya vipashio inapaswa kuonyeshwa vizuri na kwa uwazi zaidi. Ubainishaji wa hadhi ya vipengele vya kileksia ndio utakaoonyesha ni vipashio vipi vinamiliki vipi katika sentensi au kirai. Aidha ubainishaji huo ndio utakaodhihirisha vipashio vilivyo katika ngazi sawa au kuwa na uhusiano wa udada. Kichwa cha kirai huwakilishwa kwa X. Hii ndiyo ngazi ya chini kabisa na huwa haina baa yoyote. Ngazi ya pili huwa na baa moja (X′) ilhali ile ya tatu huwa na baa mbili (X′′) na kuendelea hivyo kutegemea muundo kirai.

**(iii) Kipambanuzi**

Kipambanuzi ni kipashio kinachobeba maneno ambayo kimuundo si lazima yawepo katika kirai. Kuhusishwa kwa maneno hayo hukusudia tu kufafanua neno kuu. Aghalabu vivumishi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika kirai nomino ilhali vielezi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika kirai kitenzi. Katlka sentensi "Msichana yule mwenye maringo amenunua vipodozi vingi sana: kipambanuzi ni kivumishi kionyeshi ñYuleò ambalo linafafanua nomino msichana.

**(iv) Kijalizo**

Kijalizo ni sehemu ya kirai ambayo huwa imeunganishwa kwa karibu sana na kichwa cha kirai hicho. Kila aina ya kirai huwa na kijalizo chake. Kijalizo huwa na uhusiano wa udada na kichwa cha kirai. Kwa mfano katika sentensi, "Juma ni mwerevu." Kijalizo kinatokea kwenye kirai kitenzi. Kijalizo hicho ni kivumishi "mwerevu."

**(v) Kipanuzi**

Kipanuzi ni sehemu ya kirai ambayo hutoa maelezo zaidi kuhusu kirai. Huwa hakina uhusiano na kichwa, kipambanuzi au kijalizo. Kwa mfano katika kirai nomino cha

sentensi: Msichana yule mwenye maringo amenunua vipodozi vingi sana. Kipanuzi ni "mwenye maringo." Kirai kinaweza kubeba kipanuzi kimoja, viwili, vitatu au zaidi. Kwa mfano, Msichana yule mwenye maringo, ambaye ni mfupi, aliye karibu na duka, amenunua vipodozi vingi sana." sentensi ifuatayo ina kichwa, kipambanuzi na kipanuzi:

**Watoto wengine wenye matatizo ya kiakili** watapewa dawa nyingi sana.

KN hiki kinaweza kuwakilishwa kwa mujibu wa X-baa kama ifuatavyo:




Nomino ñwatotoò ni kichwa ambacho kinatawala kipambanuzi ñwengineò na kipanuzi ñwenye matatizo ya kiafya.ò

Vivyo hivyo, KT hiki kinaweza kuwakilishwa kwa mujibu wa X-baa kama ifuatavyo:



Utafiti huu utatumia nadharia hii ya x-baa ambayo inaendana na mada yetu ya utafiti imemsaidia mtafiti kubaini aina ya vishazi tegemezi vinavyojitokeza katika lugha ya kisukumu na kuviainisha kwa kuzingatia miundo yake na pia  kuvichanganua kwa kutumia njia ya ngoe / mchoroti ambapo kifundo kimoja kigawike mara mbili.  Na hivyo nadharia hii imekuwa dira katika uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha kisukuma.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii imetoa taarifa mbalimbali zinazohusiana mada ya utafiti ambayo ni uchanganuzi wa kishazi tegemezi cha kisukuma. Mtafiti amesoma majarida, vitabu, na tafiti kadhaa zilizokwishafanyika juu ya mada ya utafiti huu ili kuweza kubaini pengo na kushadidia data za utafiti wetu.

# SURA YA TATU

# MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

**Seh**emu hii inaelezea mbinu mbalimbali za utafiti ambazo zimewezesha kupatikana kwa data za awali (msingi) na za upili Mambo yanayowasilishwa katika sehemu hii ni Eneo la utafiti, Kundi lengwa, Sampuli na usampulishaji wa kundi lengwa, mchakato wa usampulishaji, mbinu za kukusanyia na kuzichambulia data,mbunu za za kuchanganulia data, Udhibiti wa mbinu za kukusanyia data na changamoto zilizojitokeza na namna kuzitatua changamoto hizo.

## 3.2 Eneo la Utafiti

**U**tafit huu umefanyika katika Mkoa wa Geita.Wilaya ya Geita Vijijini katika Tarafa ya Butundwe. Katika shule ya sekondari Bukondo, Nyachiluluma, Chigunga, Butundwe, Katoro, nyamigota, Lutozo, Kaseme na vijiji vya maeneo hayo. Maeneo hayo yamependelewa kwa sababu mtafiti anauzoefu nalo na ni eneo ambalo linawazungumzaji wengi wa kisukuma ambao hawajaathiriwa zaidi na lugha nyingine na walimu wanaofundisha shule za upili somo la Kiswahili wanapatikana kwa urahisi.

## 3.3 Kundi Lengwa

**A**damu (2008) anaeleza kuwa ni vigumu kwa mtafiti kushughulikiwa idadi ya wanajamii wanaohusika katika utafiti hata kama anaona watafitiwa wote ni muhimu. Mtafiti hutakiwa kuchagua idadi maalumu ya wanajamii wa kushughulikia katika utafiti wake.

Kwa mujibu wa Williman (2011) anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti (vinavyotafitiwa). Kwa ujumla kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Hivyo kundi lengwa katika utafiti huu ni walimu, wazee wa vijiji na wanafunzi wa shule za Sekondari Bukondo, Nyachiluluma, Chigunga, Butundwe, Kaseme, Lutozo na Nyamigota pamoja na walimu wanaofundisha somo la Kiswahili. Walengwa hawa wamependekezwa kwa sababu ndio wenye uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika katika utafiti huu. Samarin (1967) anaeleza kuwa watafitiwa katika usomi wa isimu huhakikisha kuwa data inayokusanywa ni miuundo ambayo wazungumzaji asilia hutamka. Watafitiwa waliochaguliwa kwa sababu ya umilisi wao wa lugha ya kisukuma isipokuwa walimu ambao wanaumilisi wa Kiswahili. Walimu wamilisi wa kiswahili waliteuliwa kwa sababu taaluma ya sintakisia ya kishazi tegemezi cha kisukuma katika uchanganuzi wake unahitaji uelewa wa kutosha .Chomsky (1965) anaeleza kuwa data inayotolewa kwa wazungumzaji asilia inaweza kutoa hali halisi ya lugha.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji wa Kundi Lengwa

Kothari (2004) anafafanua sampuli kuwa ni kundi dogo la watafutiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa kwalo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake. Utafiti huu umehusisha sampuli ya watu 98 wanafunzi wakiwa 60 walimu 30 na pia wazee 8 wenye umri wa kiuanzia miaka 45-75. Mtafiti alichagua umri huu kwa sababu wao ndio wanaotumia kisukuma halisi. Kigezo cha umilisi wa lugha ya kisukuma na elimu kilizingatiwa kaitka uteuzi wa sampuli kwa sababu Taaluma ya sintakisia ya uchanganuzi wa vishazi tegemezi vya kisukuma inahitajika ndiyo maana

wakateulia walimu wanaofundisha Kiswahili na wanafunzi pia wanaosoma Kiswahili. Mgawanyo wa sampuli unaowasilishwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Sampuli ya Watafitiwa**

| **Sampuli** | **Idadi** | **Walioshiriki** |
|---|---|---|
| Wanafunzi | 60 | 60 |
| Walimu | 30 | 22 |
| Wazee | 8 | 8 |
| **Jumla** | **98** | **90** |

### 3.5 Maadili ya Utafiti

Ili kuweza kufanikisha utafiti wake mtafiti ,mtafiti ni lazima aeleze maadili ya utafiti ili aweze kutoa taarifa za ukweli na za uhakika. Madili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa usiri yaani mtafiti kutotoa siri za watafitiwa. Pia kuwahakikishia usalama wao watafitiwa, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti,haki ya kujibu swali waliopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Watafitiwa walijibu maswali waliyopenda kujibu.

### 3.6 Mchakato wa Usampulishaji

Kwa mujibu wa Sigh (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafutiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Sampuli huchaguliwa kwa njia mbalimbali ikiwa pamoja na nasibu na isiyo nasibu.Ruane (2005) anafafanua usampulishaji nasibu kuwa ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua memba yeyote katika kundi lengwa huwa mkubwa. Usampulishaji usio nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambayo huegemea zaidi maamuzi ya mtafiti huweza kutoa matokeo jumuishi

kuhusiana na kundi lengwa.yaani mbinu ya kuchagua sampuli ambayo sehemu ya watafitiwa huchaguliwa kwa kuzingatia zaidi upatikanaji wao kuliko uwakilishi wao.

Moja kati ya sampuli inayopatikana kwa njia hii ni sampuli ya makusudi. Sampuli ya makusudi ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa. Mugenda na Mugenda (2003) Wanasema kuwa mbinu hii inamruhusu mtafiti kutumia watu, vitu, hali au tabia ambazo zinataarifa inayohitajika kwa kuzingatia malengo ya utafiti wake. Wanaendelea kusema kuwa mbinu hii inaweza kuambatana na matumizi ya mbinu nyingine ili kupata sampuli halisi. Usampulishaji wa makusudi ni uteuzi wa moja kwa moja wa sampuli yenye sifa lengwa. Tumeteua kimakusudi watafutiwa ambao ni wazee, wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili kutoka kwa sampuli kubwa ya walimu.Walimu walioteuliwa ni walimu wa kiwango cha shule ya upili. Tumependelea sampuli hii kwa sababu ya kiwango chake cha utendaji katika matumizi ya Kiswahili.

Walimu wa kiswahili katika kiwango cha shule za sekondari hujikita zaidi katika ufundishaji wa dhana ya kirai, kishazi na sentensi za Kiswahili. Kwa hiyo tunatarajia kuwa kutokana na tajriba na kiwango chao cha usomi wa lugha, walimu lengwa wanautendaji mkubwa katika Kiswahili na hivyo tutazalisha data muwafaka kwa utafiti wetu. Katika utafiti huu mbinu ya makusudi ilitumika kuteua shule za kutafitiwa kwani shule husika ziliteuliwa makusudi kutegemea hasa lahaja ya Kisukuma, maeneo ambayo Wasukuma wanapatikana kwa wingi pamoja na maeneo yanayoonekana kwamba hayajaathiriwa sana na lugha nyingine zinazopatikana lugha hii ya kisukuma. Watu waliohojiwa waliteuliwa makusudi kwa kuzingatia kigezo cha wenye kumudu vyema lugha ya Kisukuma. Hata hivyo mbinu hii haingeweza

kutumiwa kuwapata watu hao wanaoimudu vyema lugha ya Kisukuma.Kutokana na hali hiyo mbinu ya usampulishaji Mpokezano ilihitajika ili kuipata sampuli inayofaa (faafu).

### 3.6.1 Mbinu ya Usampulishaji Mpokezano

Mbinu hii hutumika pale ambapo vyanzo mahususi vya taarifa zinazohitajika katika utafiti hazifahamiki vizuri. Kwa hiyo Watu (sampuli) wa chache huweza kutumiwa kuwataja wengine wanaowafahamu kuwa wana data inayofahamika. Mbinu hii ilitumiwa kuwauliza baadhi ya wanafunzi, wazee na walimu katika shule,vijiji ili waweze kuwatambulisha wenzao wanaomudu vyema lugha ya kisukuma kwa ajili ya kushiriki katika utafiti huu. Matumizi ya mbinu hii yalirahisisha upatikanaji wa watu hao kwa kuwa wanafunzi,walimu na wazee wa maeneo hayo wanajua wenzao ambao wanauwezo mkubwa wa kutumia lugha ya kisukuma.Kwa ujumla matumizi ya mbinu ya makusudi na Usampulishaji Mpokezano yaliwezesha kupata Sampuli yenye kukidhi malengo ya utafiti huu.

Utafiti huu umetumia sampuli ya makusudi inayochaguliwa kwa njia ya usampulishaji usio nasibu.mtafiti ametumia aina hii ya sampuli katika utafiti huu kwa sababu tuliamini kuwa kundi hilo ndilo lenye uwezo wa kutoa taarifa itakayofaa (faafu) na wakilishi kwa kundi lengwa katika utafiti.

## 3.7 Mbinu za Kukusanyia na Kuchambulia Data

Katika utafiti huu mbinu mbalimbali zitatumika katika kukusanya data na kuzichambua. Mbinu za utafiti zinafafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti ziko katika makundi

makubwa matatu ambayo ni mbinu za kukusanyia data, mbinu za kuchanganua data na kuwasilisha data.

### 3.8 Mbinu za Kukusanyia Data

Mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti amezitumia ili kupata data za utafiti.Ni muhimu kusisitiza kwamba uteuzi wa ala ya kukusanyia data utategemea ,Suala la utafiti,Madhumuni na malengo ya utafiti.aina na kiasi cha data/sampuli, Nadhariatete za utafiti na Upeo wa utafiti.

Kothari (1990) anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusanya ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Aidha mtaalamu huyu anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data.

Utafiti huu umeufanyika kwa kuzingatia mawanda mawili yaani utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani. Katika utafiti wa maktabani mtafiti alidurusu vitabu, majarida, majuzuu na tasnifu, usomaji wa maktabani ulimwezesha mtafiti kudhibiti ubora zaidi wa taarifa za kinadharia kuhusu mada za kishazi tegemezi na kuweka msingi wa utafiti.Tumesoma vitabu vinavyohusu nadharia ya X ï Baa ninayotumia ili niweze kuielewa zaidi na jinsi ya kuitumia katika utafiti huu. Tumesoma pia kazi zilizoandikwa kuhusu kishazi tegemezi kwa ujumla ili kujue waziwazi maana ya kishazi tegemezi,maumbo yake, aina zake na jukumu lake katika sentensi.Katika kusoma huku amehakikisha kuwa amechuja mawazo ya wasomi wengine ili

kuyalinganishe na kuyalinganua na mawazo ya mtafiti. Baada ya kuweka msingi wa utafiti,mtafiti alitekeleza utafiti wa nyanjani kuhusu mada ya kishazi tegemezi cha kisukuma. Utafiti wa nyanjani ulihusisha hatua tatu za kijumla; ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, na uwasilishaji wa data kwa kutumia mbinu hizo hojaji na, mahojiano.

### 3.8.1 Hojaji

Goods na Hatt (1959) wanaeleza kuwa, hojaji ni seti ya maswali yaliyoandikwa au kauli zinazohusiana na suala linalotafitiwa ambayo mtafiti hutoa kwa wasailiwa kwa minajili ya kuibua habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahususi kuhusu mada ya utafiti.Kwa kifupi, hojaji ni orodha ya maswali au mambo yanayohitaji kujibiwa au kuelezwa na wahojiwa kwa lengo la kukusanya taarifa (Data) Maswali haya yanatakiwa kuwa mafupi na kila swali lilenge jambo moja lisiulize mambo mengi. Hojaji hujumuisha maswali yaliyotungwa kwa njia maalumu ili kutolewa kwa sampuli ya wasailiwa waliolengwa katika utafiti Fulani.Kuna aina mbili kuu za maswali.

**Maswali funge** – Haya ni maswali ambayo mtafiti humfungia msailiwa kwa kumwekea orodha ya majibu ili achague mojawapo. Maswali haya huwa ni rahisi kuyajibu, huhitaji muda mfupi kuyajibu na humfungia msailiwa ndani ya mipaka ya mada husika.Na pia matokeo huwa ni rahisi kujedwalishwa na kuchanganuliwa. Maswali ya aina hii hayampi msailiwa fursa ya kujieleza na kufafanua majibu pia na kutoa maoni yake.

**Maswali wazi –Ni** aina ya maswali ambayo humpa msailiwa nafasi ya kutoa maoni na hata kufafanua maoni hayo kwa lugha yake au kwa maneno yake mwenyewe. Kwa

ujumla maswali yote ya hojaji yanatakiwa. Yalenge kutimiza madhumuni ya utafiti, yalenge kujibu maswali ya utafiti,yalenge kuthibitish na kubatilisha nadhariatete za utafiti, yawe katika lugha rahisi yenye kueleweka, yasiwe ya kuchanganya na kusababisha kuibua zaidi ya jibu moja.

Maswali yaliwasilishwa kwa wasailiwa ambao ni wazee,wanafunzi na waalimu kwa lugha ya Kiswahili na kisukuma. Maswali yaliulizwa yanayohusiana na vishazi tegemezi vya kisukuma na yaliweza kujibiwa kwa mdomo na kwa maandishi kwa wakati ule ule Mtafiti alitoa fursa ya watafitiwa waliosoma na wasiosoma kushiriki katika kutoa taarifa.

### 3.8.2 Mahojiano

Ni mazungumzo rasmi ya ana kwa ana baina ya mtafiti na mhojiwa au wahojiwa kwa minajili ya kuibua habari maalumu inayohitajika katika utafiti. Kwa mujibu wa Kothari (2009) mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti huwauliza watafitiwa maswali na wakati mwingine watafitiwa nao huuliza maswali na mtafiti huyajibu mbinu hii ilitumika kwa watafitiwa 20. Kumi (10) kwa wanafunzi wa kidato cha tatu na nne na kumi (10) kwa walimu. Mahojiano haya yalifanyika punde tu baada ya watafitiwa kumaliza kujaza hojaji mbinu hii iliteuliwa kwa sababu ya kupata uthabiti wa majibu ya watafitiwa pamoja na kupata uthabiti wa mbinu za kukusanyia data.

Pili. ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli kwa usahihi zaidi. Hii iliwezekana kwa sababu mtafiti alikutana na wahojiwa ana kwa ana na kuwauliza maswali na kurekodi majibu yao.Maswali yaliyokosa majibu yalitafutiwa ufumbuzi papo kwa papo.

Tatu ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi kwa sababu watafitiwa wanaweza kuuliza maswali na mtafiti anakuwa na uhuru wa kuuliza maswali ya ziada ambayo ni vigumu kufanyika kwa kutumia mbinu nyingine kama vile ushuhudiaji ushiriki au hojaji. Baadhi ya wahojiwa nitawahoji kwa simu hii ni kulingana na majukumu waliyonayo, kwanza mtafiti alitayarisha maswali ya mahojiano,pili mtafiti alihakikisha kuwa mhojiwa amelielewa swali, alijitahidi kumpa mhojiwa muda kujibu na kujieleza.tatu alijenga uhusiano mzuri na mhojiwa na hii ilimsaidia kumpa mhojiwa achague wakati unaomfaa mhojiwa kumhoji. Amenuia kutumia mbinu ya mahojiano ya simu kwa baadhi ya wahojiwa kwa sababu zifuatazo: Kwanza, inampa uhakika kwamba walengwa wake ndio waliojibu maswali.

Pili itamsaidia kuuliza ufafanuzi wa majibu yasiyoeleweka.

Tatu, itamsaidia kukusanya data kwa walengwa wasojua kusoma.

Nne, itamsaidia kujua mipaka ya kutokuruka malengo yaliyokusudiwa.

Tano, mbinu hii husaidia kumtathmini msailiwa na kubadilisha mbinu inavyopaswa. Na waliobaki nitawauliza maswali ya ana kwa ana.Mahojiano haya yalifanikiwa kwa urahisi kwa sababu wasukuma wanamudu pia Kiswahili.Data waliyokuwa wanaitoa ilijazwa na mtafiti mwenyewe.

## 3.9 Mbinu za Kuchanganulia Data

Data katika utafiti huchanganuliwa kwa kutumia mikabala ya aina tatu . mkabala wa kiidadi, mkabala usio wa kiidadi na mkabala wa kidhamira. Enon, (1998) anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa maelezo kwa sababu kulikuwa na data zilizotokana na majibu ya kimaelezo yanayogusa maoni ya wahojiwa Ilhali Mtafiti alitumia mkabala

wa kiidadi kwa lengo la kupata takwimu sahihi za data.Taaluma ya takwimu ina dhima maalum katika utafiti wa aina yoyote. Gupta (1986:.1.11) anasema dhima za takwimu ni kama ifuatavyo:

-Kumwezesha mtafiti kupata habari kwa uhakika ,. -Kumwezesha mtafiti kupata mpango mzuri na dhahiri wa data iliyokusanywa., -Kumwezesha mtafiti kulinganisha data., -Kumwezesha mtafiti kuzua nadharia mwafaka na vilevile kuifanyia majaribio nadharia yake,.- Kumpa mtafiti uwezo wa kubashiri,-Kumpa mtafiti uwezo wa kuibua maamuzi,sera au mwongozo mwuafaka. Kwa mujibu wa Gupta (1986:16) anasema umuhimu wa takwimu kuwa,kwa kweli hapana kazi yoyote ya utafiti leo ambayo itakamilika bila data za kitakwimu na njia za kitakwimu. Katika utafiti huu ulitumia mikabala yote miwili.

Kwa kuwa mtafiti ni mmilisi wa wa lugha ya kiswahili ametumia tajriba yake katika lugha ya kiswahili ili kuvichambua vishazi tegemezi vilivyochanganuliwa kuhusu lugha ya kisukuma. Baada ya usomaji wa kina kama msomi wa Kiswahili alipata data yake kwa kutunga sentensi zenye vishazi tegemezi vya kisukuma na kutumia na nadharia ya X- Baa kuchanganua. Vishazi tegemezi alivyovitunga vilitathiminiwa na wasomi wenzetu ili kuthibitishwa usahihi wake.

Alitumia uchanganuzi wa X-Baa kudhihirisha ufaafu wa nadharia ya X-Baa katika uchanganuzi wa data husika.Na mkabala wa dhamira ulitumika katika uchambuzi wa data za utafiti kwa kuzingatia hatua zake nne ambazo ni kupanga data zinazofanana katika kundi moja, kuunda mada kuu na ndogo ambazo zilitumika katika uchambuzi wa data,kuuoanisha mada kuu na ndogo ilizilete uwiano mzuri katika uchambuzi na mwisho ni kuchambua data.

### 3.9.1 Udhati wa Mbinu za Kukusayia Data

Moja kati ya sifa kuu ya data ni kupata udhabiti wa data hizo. Kothari (2004) amefafanua kuwa udhabiti ni kiwango ambacho mbinu za utafiti zitapima kile kilichotakiwa kupimwa na mbinu hiyo.Naye sigh (2007) anasisitiza kuwa zana/mbinu zote zilizotayarishwa kwa ajili ya kufanyia utafiti lazima zipimwe ili kuona kuwa zinafaa katika mazingira halisi yaliyokusudiwa. Kwa msingi huo mtafiti aliamua kuzipima hojaji kwa watu ambao sio walengwa wa utafiti huu lakini wanafanana katika viwango vyao vya Elimu kabla ya data kukusanywa.

Lengo la kupima hojaji ni kutaka kujua iwapo maswali yanafahamika kwa watafitiwa.Pia kujua iwapo mtafiti atapata taarifa anazohitaji kulingana na utafiti wake.Hivyo baada ya kuzipima hojaji mtafiti alipata fursa ya kufanya marekebisho pale palipohitajika ili kuziboresha zaidi kabla ya kuzigawa kwa Watafitiwa waliokusudiwa kwa kwa ajili ya kukusanya data za utafiti.Katika utafiti huu hojaji zimejaribiwa kwa Wanafunzi wa kidato cha nne,tatu na Walimu wa shule ya sekondari Bukondo.

## 3.10 Changamano Wakati wa Kukusanyia Data

Utafiti huu umefanywa kwa muda uliopangwa na matokeo yamepatikana. Changamoto zifuatazo zilijitokeza. Mosi, ugumu wa kupata watafitiwa wakati wa kukusanya data kwani wakati ulipofika baadhi ya wanafunzi walikuwa katika mitihani ya utimilifu (mock) hasa kidato cha nne. Hata hivyo halikuwa tatizo kubwa katika utafiti huu kwani idadi iliongezwa kwa Wanafunzi waliopatikana wa kidato cha tatu. Ili kukidhi mahitaji ya utafiti. Pili, utafiti huu pia umekabiliana na changamoto ya kutafsiri sentensi kutoka katika Kisukuma hadi Kiswahili.Tatizo hili mtafiti aliweza

kukabiliana nalo kwa kutumia tajiriba aliyonayo kutokana na kusoma kozi hiyo katika shahada yake ya kwanza.

Tatu, baadhi ya watafitiwa kukataa kutoa maelezo kwa kumwogopa mtafiti jambo hili lilifanya utafiti kuchukua muda mrefu.Na hapa ndipo Elimu ilipohitajika ya kuwaelimisha kuhusu malengo ya utafiti huu na kuwambia kuwa majibu watakayo toa ni siri. Na utafiti huu ni wa kielimu si wa kibiashara. Nne baadhi ya hojaji walizopewa watafitiwa hazikurejeshwa hapa ilibidi kutoa hojaji nyingine zaidi na baadhi ya walimu kuwepa kujibu swali la sita.

### 3.11 Hitimisho

Sura hii imefafanua namna utafiti ulivyofanyika. Sura imegawanyika katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza inaeleza eneo la utafiti. Sehemu ya pili inafafanua kundi lengwa.Sehemu ya tatu inaeleza sampuli na usampulishaji wa kundi lengwa.Sehemu ya nne inaeleza mchakato wa usampulishaji.Sehemu ya tano inaeleza mbinu za kukusanyia na kuchambulia Data. Sehemu ya saba inaeleza Udhabiti wa mbinu za kukusanyia data.sehemu ya nane inaeleza changamoto zilizojitokeza wakati wa kukusanya data na namna ya kuzitatua.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii data zimewasilishwa zilizopatikana katika eneo la utafiti. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya x-baa ambapo vishazi tegemezi huchangauliwa kwa kuzingatia kategoria na kila kishazi tegemezi kinamilikiwa na kichwa .Uchanganuzi na uchambuzi huu wa data umelenga kujibu maswali ya utafiti huu na kuweza kukamilisha malengo ya utafiti.Maswali ya utafiti huu.

## 4.2 Kubainisha Vishazi Tegemezi vya Kisukuma

Radford (1988) anasema kila kirai kinakichwa kinachoamua sifa za kirai chote na huainishwa kimuundo kulingana na neno kuu.kirai ambacho neno kuu ni nomino au kitenzi huitwa kirai nomino au kirai kitenzi. Katika nadharia ya X-Baa virai vyote vinatawaliwa na neno kuu yaani X. Maneno haya makuu ni vitengo vya chini kabisa na hutawala maneno mengine. Maelezo haya yamemsaidia mtafiti katika kubaini virai viavyoungana kuunda vishazi tegemezi vinavyojitokeza katika lugha ya Kisukuma kwa kuzingatia sifa ya kishazi husika.Navyo vinabainishwa kama ifuatavyo:

| **Kisuma** | **kiswahili** |
|---|---|

Bhanakijiji abhobhakiandikisha =Wanakijiji waliojiandikisha

Shitabo isoshigelile = Kitabu kilichopatikana

Gwibhi *uyoakapigwa* risase = Mwizi aliyepigwa risasi

Nigini *uluulilila* Lugembe gwinhage = Mtoto akililia wembe mpe

Linti *ilyabhugwe* gwibharabhara = Mti ulioanguka barabarani

Ibhabhayu *ilyabhuhye* = Papai lililoiva

Isumbe *ilyabhipile* =Kiti kilichoharibika

Sumba *uyoakatumwa* =Kijana aliyetumwa

Bhanafunzi bhakatupija *,ahobhatubona = wanafunzi walitufukuza,walipotuona*

*Umoakingilila* tukimila = Alivyoingia tulisimama

Gwalimu *uyoalilanga* = mwalimu anayefundisha

Bhageni *abhobaking*a = Wageni walioondoka

Masanja akasatwa *umokalilila* = Masanja alimuhurumia alivyolia

*Ahotwinga* bhakalugala unyango = Tulipotoka walifunga mlango

Bhakalila *kunguno ya* kogoha = walilia kwa sababu waliogopa

Ngôoma iye itulila *kulwene* itandukile =Ngoma hii hailii kwa kuwa imepasuka

Numba *iyoizengilwe* gwibonde = nyumba iliyojengwa bondeni

**B**hageni *abhobakiza* igolo = Wageni waliokuja jana

Madoke *agabuhye* genhagwa lelo = Ndizi zilizoiva zimeletwa leo

Shilatu *ishowazwalaga* shitafulile =kiatu alichovaa hakikufuliwa

Mashamba *ayogalimagwa* agatahambile =Mashamba yaliyolimwa hayajapandwa

Ilunde *ilolilitukundikijaga* no =wingu linalotugubika sana

Bhebe uyouhamanile = Wewe unayepafahamu

Chupa iyoekatanduka = Chupa iliyovunjika

Gwene, sumba uyowalusimbilaga = Yeye ,kijana anayechimbia

Bhebe, mwanafunzi *uyoutiyambaga* = Wewe,mwanafunzi usiyejitahidi

Myele *uyoakenha* kalamu washikaga = mzazi aliyeleta kalamu amekwisha fika.

Maliwa *ayo gakasimbiwa* gatahile shiza = Mihogo iliyochimbwa haikuiva vizuri

Kabudi *iyoikafulwa* yumaga = koti lililofuliwa limekauka.

Mifano iliyotolewa hapo juu ni mifano ya vishazi mbalimbali vya kisukuma ambavyo vimekitwa katika vitenzi. Maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo ndicho chimbuko la uhusiano uliopo katika maneno yote yanayohusika katika kila kishazi. Ubainishaji wa kishazi tegemezi cha kisukuma unadhihirisha kuwa tungo kishazi cha kisukuma kina maumbo na miundo mbalimbali kulingana na vishazi vilivyomo katika kisukuma.

## 4.3 Kubainisha Vishazi Tegemezi vya Kisukuma kwa Kuzingatia Kigezo cha Maana na Kimofolojia

Katika utafiti huu ubainishaji wa vishazi tegemezi vya kisukuma hufanyika kwa kuzingatia vigezo vikuu viwili.Yaanikwa kutumia kigezo cha maana na kigezo cha kimofolojia.

### 4.3.1 Kigezo cha Maana

Tunaweza kutambua kama kishazi fulani ni tegemezi kwa vile hakitakuwa kinatoa maana kamilli.Msomaji atabaki anajiuliza maswali kadhaa ambayo hayawezi kujibiwa kwa kusoma kishazi hicho. Mfano *Wanaolima mashamba yetu ...........Abhobalilima mashamba gise*




mwalimu aliyehamia kwetu -gwalimu uyowasamilile kubise




Chakula *kilichobaki jana.................* Shakulya ishoshikashiga igolo.

**K**atika kigezo hiki ndipo tunapata vishazi tegemezi vivumishi ambavyo vimeshushwa hadhi na kushika nafasi ya kirai nomino.Vishazi hivi hufanya kazi ya vivumishi Kuna aina mbili ya vishazi tegemezi vivumishi:

**Vishazi tegemezi vinavyoambatana na jina linalovumishwa**

| **Kisukuma** | | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| ***Ng'wanakijiji uyoakapejiwa wachaga*** | = | ***Mwanakijiji aliyefukuzwa***ameuawa. |
| *Shitabo ishoshikibiwa* shigeraga/shilongaga | = | *Kitabu kilichoibiwa* kimepatikana |
| *Mashitinde ayogakatandulwa* gagujiwagwa | = | *Magogo yaliyopasuliwa* yameuzwa. |

**Vishazi tegemezi ambavyo haviambatani na jina linalovumishwa**

| **Kisukuma** | | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| *Abobatindaga* banonhȏgwa | = | *Waliofuzu* wamezawadiwa. |
| *Abobachilagwa* bajaga | = | *Waliofiwa* wamesafiri. |

Abobigasha bemile =Waliokaa wasimame.

Maumbo yanayojitokeza kwenye vitenzi.

Yapo maumbo ambayo yakijitokeza kwenye umbo la kitenzi hufanya kishazi kiwe tegemezi.Maumbo haya kisarufi hujulikana kama "Viwakilishi Rejeshi.".Maumbo haya badala ya hukaa mwanzoni mwa kishazi kwa kuambatana na -amba- huambatanishwa kwenye mzizi wa kitenzi Hivyo maumbo haya ambayo huyatambua kama viwakilishi rejeshi ni kama vile **ye, o, yo, lo, cho, vyo. zo, po, ko, na mo nakadhalika**

### 4.3.2 Kigezo cha Kimofolojia (Maumbo)

Kuna maumbo ambayo yakijitokeza katika kishazi fulani hukifanya kishazi hicho kiwe kishazi tegemezi.Maumbo haya mara nyingi hutokeza mwanzoni mwa kishazi au kwenye umbo la kitenzi. Kwa kutumia kigezo hiki tumeweza kubaini aina zifuatazo

Vishazi tegemezi vyenye muundo wa viambishi vya wakati.

Hivi ni vishazi tegemezi ambavyo hudokezwa na matumizi ya vihusishi vya wakati. Mara nyingi vishazi rejeshi hivi huwa kama vijalizo katika sentensi kama vile hadi, kwa sababu baada ya, kabla ya, vile vile vishazi rejeshi vyenye muundo huu kiambishi óôkoôô cha mahali na óôpoôô cha hali.

| Kisukuma | Kiswahili |
|---|---|
| Bhalozi waja ukobhasinzaga embuli | = Balozi amekwenda walikochinja mbuzi. |
| Nakuyega sana Unimo uyu ulugulashile | = Nitafurahi sana kazi hii itakapomalizika. |
| *Ahikazaho umayu alizuga* | = *Wakati* mama anapika |

Aha harakati ja kwigunana = *Katika* jititahada za kujikwamua

*Tangu ahobalekane* = *Tangu* waachane

*Kwa kuwa* shati lake limepasuka.

*Ili natindele lazima nagwe bhugota.* = *Ili* nilale lazima nimeze vidonge

*Ulu atigelile.* = *Iwapo* hatatokea

Kutokana na kigezo hiki cha kimofolojia tunapata kundi la pili la kishazi tegemezi ambalo ni kishazi tegemezi kielezi. Kishazi hiki hufanya kazi ya vielezi katika sentensi.

Mfano **Kisukuma** **kiswahili**

Mayu akasaya *ahowasigwa* = Mama alichukia *aliposengenywa.*

Tukasatwa *umoakalilila.* = Tulimhurumia *alivyolia*

Bakatupeja *ahobatuona.* = Walitufukuza *walipotuona.*

Vishazi tegemezi vielezi hugawika katika aina kuu sita nazo ni kama ifuatavyo:

(a)**Vishazi tegemezi vielezi vya mahali**.Vishazi hivi hubainisha mahali kitendo kilipotendeka.Vishazi hivi huambatana na mofu ambazo hudokeza mahali kama vile {po}

Mahali dhahiri,{-ko} mahari ambapo si dhahiri, {mo} ndani ya kitu fulani

Kisukuma Kiswahili

Mfano: *Ukoakaja hatamanikile* = *Alipoenda* hapafahamiki.

*Ukoakaja ili siri ya baleli bakwe* = *Alikokwenda* ni siri ya walezi wake.

Umowalalaga halinunđha = Alimolala pananuka.

**(b) Vishazi tegemezi vya mashart**i

Hivi ni vishazi vitegemezi vinavyodokeza masharti yapasayo kutimizwa kabla kitendo hakijafanywa. Huundwa kwa viambishi vya masharti kama vile **ki, po** ya masharti**, nge, ngeli na ngali**.Huweza pia kuundwa kwa maneno/ viunganishi vya masharti kama vile kama, iwapo, ikiwa, kwa mfano.

*Ikiwa* utalima mapema, utapata mazao mengi.

Tutaondoka a*ki*ja mapema

Tungalicheza zaidi yao tungaliwashinda.

**(c) Vishazi tegemezi vya sababu**

Vishazi hivi hueleza sababu ya kufanyika kwa kitendo.Huundwa kwa viunganishi vya sababu kama vile kwani, kwa vile, kwa sababu kwa mfano:

**Kisukuma** **Kiswahili**

Uhamisi atigushaga kulwasababu akiminya Igolo = Hamisi hachezi *kwa sababu* aliumia jana.

Alilila kulwa sababu akadukilwa shaminala sana = Alilia *kwa sababu* alitusiwa vibaya.

**(d) vishazi tegemezi vya walakini/kinyume**

**Vishazi hivi** hueleza hitilafu au kasoro iliyo katika kitendo. Huundwa kwa maneno kama vile ingawa, licha ya, japo, ijapokuwa, kwa mfano:

| **Kisukuma** | | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| Tukutinda nulu habi na fufujo | = | Tutashinda *ingawa* kuna fujo |
| ***Nulu*** *bhitogilwe* bhatalitola | = | *Ingawa* wanapendana hawataoana. |
| **Nu**lu abiatina sare ya shule akwita utihani | **=** | **Japokuwa** hana sare ya shule atafanya mtihani. |

**(e) Vishazi tegemezi vya kusudi**

Vishazi hivi hueleza kusudi la kufanya jambo.Hubainishwa kwa maneno yanayoleta maana ya kusudi la kutnda jambo fulani. Kwa mfano:

*Ili tushinde mtihani wetu, lazima* tukazane zaidi.

**(f) Vishazi tegemezi vielezi vya njeo**

Hivi ni vishazi tegemezi ambavyo hubainisha muda au wakati kitendo kinapofanyika. Mofu za njeo hutumika kama vindokezo vya wakati.

| **Lugha ya kisukuma** | | **Lugha ya kiswahili** |
|---|---|---|
| Ahobasaba bhubiba ababyele bhao. | - | Walipotajirika waliwasahau wazazi wao. |
| Ulubalamale ukwimba bakubina mbina. | - | Watakapomaliza kuimba watacheza ngoma. |

**(g) Vishazi tegemezi vielezi vya jinsi**

**H**ivi ni vishazi tegemezi ambavyo hudhihirisha jinsi kitendo kilifanyika.

**Lugha ya kisukuma** **Lugha ya kiswahili**

Mfano: Umobhalibinila mbina bhalitogisha bhingi=*Wanavyocheza* ngoma wanafurahisha wengi.

*Umoalesekela alekola bhingi.* = *Anavyocheka* anaudhi wengi

**(g) Vishazi tegemezi vyenye miundo iliyokitwa katika udondoshaji wa kipashio**

Mifano ya vishazi vyenye miundo ya vipashio vilivyodondoshwa ni kama ifuatavyo:

Hapendi kuonywa wala *kushauriwa.*

Habari ile ni mbaya tena *ya kutisha*

Baba ataamua kunyamaza au *kusema*

Katika mifano hii vishazi tegemezi *kushauriwa, ya kutisha*,na *kusema.* Havi kutanguliwa vitenzi.Katika mazingira ya sentensi hizi vipashio vilivyo kiini cha habari haviwezi kurudiwa kabla ya vishazi tegemezi hivyo.

**(h) Vishazi tegemezi vielezi vya ukinzani**

Hivi ni vishazi tegemezi ambavyo huonyesha hali ya ukinzani wa matarajio.

| **Lugha ya kisukuma** | | **Lugha ya kiswahili** |
|---|---|---|
| Nulu baligusha chiza batututinda | = | Ingawa wanacheza vizuri hawatatushinda. |

Eki atinashimanhisho sha chuo agwita mazoezi. =Japokuwa hana kitambulisho cha chuo atafanya mazoezi.

Eki bitogilwe batalitola = Ingawa wanapendana hawataoana

**4.4 Kuchanganua Vishazi Tegemezi vya Kisukuma -Mtazamo wa X-baa**

Kwa mujibu wa nadharia ya X-baa vishazi huundwa kwa kuunganisha virai mbalimbali. Kila kirai kimsingi kina mvurumisho wa kichwa chake katika bar mbili ambapo baa ya pili ni ya juu kabisa na inayowakilisha kirai kamili.Hivyo katika uchanganuzi wa kirai cha lugha yoyote kwa kutumia nadharia ya X-bar ni kukigawa

kirai kwa kuzingatia mahusiano baina ya neno kuu na vipengele vingine vinavyounda kirai hicho ambapo kichwa hugawika katika matawi mawili pekee.

Ndani ya utafiti huu alama saidizi ya Xô imetumika katika kuchanganua kishazi tegemezi cha kisukuma kwa kuzingatia muundo wake. Pamoja na kuwa Watalaamu mbalimbali wamejaribu kuchanganua kishazi kwa kutumia alama saidizi tofauti ,kwa mfano Jackendoff baa tatu, Chomsky alitumia alama saidizi yenye baa moja na Radford alitumia alama saidizi ya Xô kuwakilisha neno kuu (kichwa). Njia hizi tatu ni tofauti lakini zinaeleza kitu kimoja. Hivyo uchanganuzi wa kishazitegemezi umefanyika kwa kuzingatia miundo na aina za vishazi tegemezi kama inavyoelezwa hapo chini.

## 4.5 Miuundo ya Vishazi Tegemezi vya Kibantu

Ni kishazi ambacho kimuundo na kimaana kimefungamana sana na kishazi kinachoandamana nacho katika sentensi. Massamba na wenzake (1999:127) Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho kikiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu hakiwezi kusimama peke yake kama sentensi yenye kujitegemea. Uainishaji wa vishazi hutegemea maana na maumbo yake. Na hapo ndipo tunapata kishazi tegemezi kivumishi na kishazi tegemezi kielezi.Kishazi tegemezi kivumishi hufanya kazi ya vivumishi, kuna aina mbili ya vishazi tegemezi vivumishi:

**Kishazi tegemezi kivumishi (N+βV)**

Hiki ni kishazi tegemezi kinachoambatana na jina linalovumishwa. Ni kishazi ambacho kinaundwa na nomino na kishazi tegemezi kwa mfano.

Isumbe *ilolikenhwa* Igolo = kiti kilicholetwa jana




Shitabo *ishoshikibiwa s*higeraga = kitabu kilichoibiwa kimepatikana.




**Manti ayogakabutwa gumile = miti iliyokatwa imekauka**




**Vishazi tegemezi vivumishi ( βV +T)**

Ni vishazi ambavyo haviambatani  na jina linalovumishwa.Mfano

*Abhobalalaga bhabuke* = *Waliolala* waamke.

*Uyowatolagwa wasafiriaga* = *Aliyeolewa* amesafiri

*Abhobadimagwa bhatungagwa* = *Waliokamatwa* wamefungwa










**Nomino, kitenzi na kielezi ( N+T+E)**

Madarasa ayogakamalwa wangu  = Madarasa  yaliyokamilishwa haraka

Shipolo ishoshikuliwa lelo =  kiporo kitakacholiwa leo

Kiwakilishi,nomino na kitenzi (W+N+T)

Muundo huu hujengwa na kiwakilishi,nomino na kitenzi.mifano yake ni:

**Kisukuma** **Kiswahili**

Gwene, sumba uyowalusimbelaga = Yeye ,kijana anayechimbia

Bhebe, Gwanafunzi uyotiyambaga = wewe, mwanafunzi usiyejitahidi

Vishazi tegemezi vielezi (ɓE)

Ni vishazi ambavyo vinafanyakazi ya vielezi katika tungo.Maumbo yanayoonesha utegemezi mara nyingi hutokeza mwanzoni wa kishazi au kwenye umbo la kitenzi. Navyo vinagawanyika katika aina sita kama vitakavyo changanuliwa hapo chini:

Mayu akasaya ***ahowasigwa*** = mama alichukia aliposengenywa.

Tukasatwa ***umoakalilila*** =Turimhurumia alivyolia




**Vishazi tegemezi vielezi vya mahali**

**Ni** aina nyingine ya muundo wa kishazi tegemezi kielezi kinachojitokeza katika kitenzi cha kisukuma.Vishazi hivi hubainisha mahali kitendo kilipotendeka.vishazi hivi huambatana na mofu ambazo hudokeza mahali kama vile ( po) mahali dhahiri, (ko) mahali ambapo si dhahiri ,(mo) ndani ya kitu fulani. Umoakingila halinamenzi =alimoingia pana maji.

*Ukoakaja* hatamanikile = Alipoenda hapafahamiki.

*Ukoakaja ili* siri ya bhalanhani bhakwe.

*Umowalalaga* halinundha = Alimolala pananuka




**Vishazi tegemezi vielezi vya wakati**

Hivi ni aina nyingine ya vishazi tegemezi ambavyo hubainisha muda au wakati kitendo kilipofanyika.

Tulipotoka walifunga madirisha = ***Ahotwinga*** bhakalugala madirisha.

Walipotajirika waliwasaidia wazazi wao =***Ahobhasaba*** bhakabambeleja bhabyaji bhabo.

***Ahomkita*** lwenya mkafungwa magori adatu =Mlipofanya mzaha mlifungwa magori matatu




**Vishazi tegemezi vielezi vya sababu**

Hivi ni vishazi tegemezi ambavyo hubainisha sababu ya utokeaji au utendekaji wa kitendo fulani.

Alipongezwa ***kwa sababu*** alifanya vizuri.

Nitakusamehe ***maadam*** umeomba radhi

Walilia ***kwa sababu*** waliogopa.










**Vishazi tegemezi vielezi vya masharti**

Hivi vinadokeza masharti yapaswaavyo kutimiza kabla kitendo hakijafanywa.

*Uluunahidi nukwenhela manonho =Ukiniahidi* nitakuletea zawadi

*Tukifanya mazoezi* tutafanya vizuri







**Vishazi tegemezi vielezi vya namna au jinsi-**

Hivi huonyesha jinsi kitendo kilivyofanyika ama kitu /mtu alivyo .Huundwa kwa kirejeshi **-vyo**

Umoaliganila alisisimua bhasumba = Anavyosimulia anasisimua vijana

Umoalilangila aliyeja sana = Anavyofundisha anafurahisha sana

Umobhalipelela bhalibatusesha no = Wanavyokimbia wanatuchekesha sana.




**Vishazi tegemezi vielezi vya hali, hitilafu, au kasoro iliyoko katika tendo**

*Ingawa* ninasoma nitafanya kazi

*Japokuwa* tumechelewa tutaingia mkutanoni

*Ingawa* wanapendana hawataoana




## 4.5 Viambishi Vipatanishi, Njeo, na Yambwa/Shamirisho Vinaweza kuwa Muundo Virai Kamili

Mtafiti alitaka kujua viambishi vipatanishi .njeo na Shamilisho/yambwa vinaweza kuwa muundo virai kamili. Swali hili liliulizwa katika hojaji na watafitiwa **98** walishirikishwa.Jumla ya watafitiwa wa kutoka sampuli A Ilikuwa**60** kati yao**58** sawa

na asilimia **97.** Walijibu ndiyo na watafitiwa **2** sawa na asilimia 3 walijibu hapana.Katika sampuli B watafitiwa **30** kati yao **24** sawa na asilimia **80 walijibu ndiyo** na watafitiwa **6** sawa na asilimia **20** wamejibu hapana. Kwa upande wa sampuli C jumla ya atafitiwa **8** kati yao ni **5** sawa na asilimia **62.5** walijibu ndiyo na watafitiwa **3** sawa na asilimia **37.5** walijibu hapana. Jedwali Namba 4.1 linaonyesha majibu ya watafitiwa waliojibu swali hili.

**Jedwali Na. 4.1: Viambishi Vipatanishi, Njeo, na Yambwa /Shamirisho Vinaweza kuwa Muundo Virai Kamili**

| **Sampuli ya watafitiwa** | **Ndiyo** | | **Hapana** | | **Hakujibu** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **Asilimia** | **Jumla** | **Asilimia** | **Jumla** | **Asilimia** |
| Sampuli A 60 | 58 | 95 | 2 | 5 | 0 | 0 |
| Sampuli B 30 | 24 | 85 | 6 | 15 | 0 | 0 |
| Sampuli C 8 | 6 | 75 | 2 | 25 | 0 | 0 |

Chanzo: Data kutoka uwandani (2016)

## 4.6 Tafsiri ya Matokeo

Jumla ya watafitiwa 58 sawa na asilimia 95 katika sampuli A,Watafitiwa 24 sawa na asilimia 85 katkia sampuli B. Watafitiwa 6 sawa na asilimia 75 katika sampuli C Ambao walishiriki kujaza hojaji. Idadi hii inafanya idadi ya watafitiwa walioshiriki kuwa 88 sawa na asilimi 89.7 kati ya watafitiwa wote ambao walishiriki wanaona kuwa vishazi vipatanishi, njeo, na yambwa vinaweza kuwa muundo virai kamili. Matokeo haya yanafanana na matokeo ya mwana isimu, **Jerono, P (2003)** katika utafiti wake alibainisha kwamba nadharia ya X-Baa inaweza kutumika kuonyesha miundo ya virai na pia virai vya kiuamilifu kama vile virai vipatanishi,virai njeo,virai

yambwa na virai jalizi. Aidha alibainisha kwamba viambishi awali vya mnyumbuliko wa kitenzi vinaweza kuchukuliwa kama virai kamili ambavyo kila kiambishi kinatawala mvurumisho wake.

Matokeo haya yanamshawisha mtafiti kusema kwamba viambishi awali vya mnyumbuliko wa kitenzi vinaweza kuchukuliwa kama virai kamili ambavyo kila kimoja kinatawala mvurumisho wake.Kutokana na hayo mtafiti ameweza kuonyesha kwamba virai si fungu la maneno pekee bali vinaweza kuwa mofu, au maneno yanayojisimamia.

## 4.7 Hitimisho

Katika uchambuzi wa data mtafiti ameweza kubainisha,kuchanganua na kuwasilisha vishazitegemezi vya kisukuma kwa kufuatana na malengo mahususi yake ya utafiti.Katika ubainishaji na uainishaji wa kishazi tegemezi cha kisukuma mtafiti ameweza kupata miundo na aina tofauti ya vishazi tegemezi vya kisukuma. Mtafiti ameonyesha vishazitegemezi vya kisukuma vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya X-Baa. Matokeo hayo yamedhihirisha kuwa kishazi tegemezi cha kisukuma kinaweza kubainishwa, kuainishwa na kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hii ya X-Baa kwa kuzingatia maana na miundo yake.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI WA MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Hii ndiyo sura ya mwisho katika utafiti huu ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Katika Sura hii ndimo mnamofanyika muhtasari wa utafiti wote na kisha, hitimisho linalohusu malengo mahususi ya utafiti linatolewa. Baada ya hapo tunatoa mapendekezo kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Katika mabunio tulitarajia kuwa tafsiri ya Kishazi tegemezi ni pana zaidi kuliko ilivyoelezwa na wanaisimu wa Kiswahili.Tumegundua kuwa dhana ya kishazi tegemezi hueleweka kwa kuzingatia kigezo kilichotumika. Tumethibitisha pia kuwa kishazi tegemezi si kikumushi cha kirai nomino au kiwakilishi pekee bali ni kikumushi cha kirai nomino,kirai kiwakilishi,kirai kitenzi ,kitenzi jina na kishazi tegemezi kingine.Mtafiti amebaini kwamba viambishi awali vya mnyumbuliko wa kitenzi vinaweza kuchukuliwa kama virai kamili ambavyo kila kimoja kinatawala mvurumisho wake.

Mtafiti alidhamiria kuwa nadharia ya x-baa ingefaa katika kuchanganua kishazi tegemezi cha kisukuma matokeo ni kuwa kwa hakika nadharia ya X-Baa ilifaa sana katika uchanganuzi wa kishazi tegemezi. Nadharia ya X-Baa inatambua nafasi ya kishazi tegemezi katika kirai na nafasi ya hiyo kuwa kimefunganishwa na kichwa cha kirai. Dhima ya kishazi tegemezi katika nadharia ya x-baa ni kupanua kichwa cha kirai hadi kiwango kingine. Hupanua ( X hadi X‶) Mtafiti ameweza kubainisha kwamba nadharia ya X-Baa inaweza kutumika katika kuonyesha muundo wa kishazi tegemezi na hivyo kudhihirisha ubia wake.

## 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umeweza kubainisha makundi ya vishazi tegemezi yanavyojitokeza katika lugha ya Kisukuma na kuviainisha vishazi tegemezi hivyo kwa mazingatio ya miundo yake na mahusiano yaliyopo baina ya neno kuu na maneno mengine katika kujenga .Huu ni mchango mkubwa katika taaluma hii sintakisia. Utafiti huu umeongeza idadi ya tafiti na maandiko ambayo yatatumika kama marejeleo wa wanaisimu wa sasa na wajao katika uchanganuzi wa vishazi tegemezi vya lugha za kibantu kwa kutumia nadharia ya X-Baa.

Utafiti huu ni msaada mkubwa kwa wanataaluma wa sintakisia ya uchanganuzi wa sentensi. Vishazi tegemezi na virai kwa kuwa itawasaidia kupata maarifa mapya yanayohusiana uchanganuzi wa sentensi na vishazi tegemezi vya lugha nyingine za kibantu kwa kutumia nadharia hii ya X-baa. Kwani utafiti huu umweza kuchanganua vishazi tegemezi vya kisukuma kwa kutumia nadharia hii ya X-baa.

## 5.4 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Fatizi

Katika utafiti huu tumeona mapengo kadha yanayohitaji kujazwa.tumegundua kuwa sentensi sharti na sentensi changamano za kisukuma zinasitahili kufanyiwa utafiti wa kina kwa kutumia nadhari ya X-Baa. Utafiti haukuweza kuchanganua vishazi huru vya kisukuma na kushughulikia aina nyingine za tungo zilizomo katika tungo hiyo.Mtafiti anapendekeza watafiti wengine wa taaluma ya sintakisia ya uchanganuzi wa sentensi kufanya utafiti.

Mtafiti anapendekeza utafiti mwengine ufanyike katika vishazi tegemezi vya lugha nyingine za kibantu ambazo hazijaweza kufanyiwa utafiti huo ili kuweza kubainisha, kuainisha na kuchanganua vishazi tegemezi hivyo kwa kutumia nadharia ya X-Baa.

## 5.5 Hitimisho

Utafiti wetu umehusu uchanganuzi wa kishazi Tegemezi cha Kisukuma kwa msingi wa nadharia ya X-Baa. Mtafiti amechanganua miundo tofauti ya kishazi Tegemezi vya kisukuma na aina zake tukizingatia nadharia ya X-Baa. Mtafiti ametumia kielelezo Tungo kufafanua kishazi tegemezi cha kisukuma.Katika Kishazi tegemezi cha kisukuma tumebaini kuwa viambishi vinavyoonesha utegemezi hupachikwa mwanzoni mwa vitenzi mfano umoakalala, uyoakiza, masumbe **ayo**gakenhwa hii inakuwa tofauti kidogo na ya lugha ya Kiswahili huchukua nafasi ya tatu katika kitenzi. Mfano ali**ye**kuja. Tumetambua kuwa maana na jukumu la kishazi tegemezi hutegemea kigezo kinachotumika katika kukifafanua Idadi ya aina za vishazi tegemezi hutegemea nadharia anayotumia mtu. Mtu akitumia kigezo cha mofolojia na maana kuna aina mbili na hivi vyote huwa na o-rejeshi ndani yake Katika lugha ya kisukuma viambishi vinavyoonyesha o-rejeshi ni vichache mfano **ayo, ilo. abo, uyu, ulu, ako, umo, uko, ejo, isho, uyo, aho, uto nakadhalika.** ukilinganisha na vya Kiswahili lakini pia kishazi tegemezi cha masharti huwa katika sehemu moja tu mfano KSKM **ulu**ninamane niniza-KSW N**inge**jua ni**nge**kuja.Unapotumia nadharia ya X-Baa aina za kishazi tegemezi ni kishazi tegemezi cha masharti,kishazi tegemezi cha sababu, kishazi tegemezi cha walakini,na kishazi tegemezi cha kusudi.na kishazi tegemezi kivumishi/kirejeshi.

## MAREJELEO

Arege, T., na Matei, A. (2006). *Kunga za Kiswahili*. Nairobi: Focus Publishers.

Chomsky, N. (1965) . *Aspects of the theory of sintax.* Cambridge: M.I.T. Press.

Cowper, E. A. (1992). *A Concise introduction to syntax; Theory; The Government Binding Approach.* Chicago: Chicago University Press.

Haegeman, I. (1991). *Introduction to Government and Binding Theory*. London: Blackwell Publishers.

Haule, F., na Katunka, F. (20120). *Nadharia ya ukalimani*: Sekondari na Vyuo. Peramiho Printing Press.

Ipara, I. (2010). *Upeo wa Sarufi kwa shule za upili.* Nairobi: Oxford University Press.

Jerono, P. (2003*).* Kishazi huru Arifu cha Kiswahili; Mtazamo wa X-Baa Tasnifu ya shahada ya Uzamili chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)/

John, G., na Mduda, F. (2012). *Kiswahili: kidato cha tano na sita*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Kadeghe, M. (2006). *Kiswahili kwa shule za sekondari Tanzania*. Dar es Salaam: Jamana Printers Limited.

Kingȇi, K. (2010). *Misingi ya Isimu Jamii.* Dar es Salaam: TATAKI.

Kioko, A., na Jepkirui, M. (2010). *Spot on grammar.* Nairobi: Oxford University Press.

Kirubi, J. (2007*) .Gateway KCSE Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2002). *Nadharia ya Lugha Kiswahili*; *Kidato cha 5 na 6:* Dar- es-salaam: Afroplus Industriea Ltd.

Massamba, D. P. B. (2004*). Kamusi ya Falsafa na Isimu*. Dar-es-salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., na Hokororo, J. I. (2001). Sarufi *Miundo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Matei. A. (2008*). Sarufi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Matinde, S. R. (2012). *Dafina ya Lugha*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mdee, J. S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili*. Sekondari na vyuo. Dar es Salaam.

Dar es Salaam University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa isimu*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, A. M. (1986*). Sarufi Mpya*. Dar es Salaam: Press and Publisher Center.

Mohamed M. A. (2001). *Moderm Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mumbo, K., na Ngamia, O. (2005). *Johari ya Kiswahili*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mutinda, M. J. (2002*) , Gold Medal Kiswahili*. Nairobi: Macmillan Publishers.

Ndalu, A. (1997). *Mwangaza wa Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Radford A.( 2004). *English Syntax*: An introducation Cambridge.Cambridge University press.

Shaaban, N. (2013). *Nadharia ya Sarufi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Taasisi ya Elimu Tanzania, (1996). *Kiswahili Kidato cha Tatu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI, (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na Lugha*. Dar-es-salaam: TUKI.

Wamitila K.W.(2004) . *Chemichemi za Kiswahili* .Nairobi: Longhorn Publishers.

Wanjala S. F. (2011) *Msingi ya ukalimani na Tafsiri*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wanjala, S. F., na Kavoi, M. J. (2013*). Stadi za mawasiliano na Mbinu za kufundishia Kiswahili.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, *(2$^{nd}$ eds.).* Thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Englewood Chiffs: Prentice Hall.

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho I: Tungo kishazi tegemezi cha kisukuma vilivyotumika katika utafiti huu**

| **Kisukuma** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Abobatindaga banonhôgwa | Waliofuzu wamezawadiwa |
| Abobachilagwa bajaga | waliofiwa wamesafiri |
| Abobigashaga bemile | waliokaa wasimame |
| Ahikazaho umayu alizuga | wakati mama anapika |
| Tangu bhalekane | Tangu waachane. |
| Uluatigelile | iwapo hatatokea |
| Tukasatwa | Tulimhurumia alivyolia |
| Bhakatupeja ahobatubona | walitufukuza walipotuona |
| Ukoakaja hatamanikile | alipoenda hapafahamiki |
| Ukoakaja ilisiri ya bhalezi bakwe | Alikokwenda ni siri ya walezi wake |
| Umowalalaga halinunôha | Alimolala pananuka |
| Ahikaza bhanajeshi balita mazoezi | Wakati wanajeshi wakifanya mazoezi |
| Bhatianalyo eli nulu elo | Hawana hili wala lile |
| Mbuli eyoikagulwa igolo yachaga | Mbuzi aliyenunuliwa jana amekufa |
| Mayu akayomba giki akwiza ntondo | Mama alisema kuwa atakuja kesho |
| Isumbe ilolikenhwa igolo | kiti kilicholetwa jana |
| Umoakingila | alimoingia |
| Numbu ijo ukasemba jaboraga | viazi ulivyochimba vimeoza |
| Kwigusha ukogutamanikile | kucheza kusikoeleweka |
| Gwene sumba uyowalusimbilaga | Yeye, kijana anayechimba |

Bhebe uyouhamanile wewe unayepafahamu

Abhobalilima mashamba gise Wanaolima mashamba yetu

Gwalimu uyowasamili habhise Mwalimu aliyehamia kwetu

Shakulya ishoshikashiga igoro chakula kilichobaki jana

Abobatindaga banonhôgwa waliofuzu wamezawadiwa

Abobigasha bemile waliokaa wasimame

Ahikazaho umayu alizuga wakati mama anapika

Ulu atigelile iwapo hatapatikana

Tangu balekane Tangu waachane

Ukoakaja hatamanikile alipoenda hapafahamiki

Umowalalaga halinunôha Alimolala pananuka

Hamisi atigushaga kulwa sababu akiminya igolo Hamis hachezi kwa sababu aliumia jana

Nulu bhitogilwe bhatilitola Ingawa wanapendana hawataoana

Babyele abobakenha kalamu bashikaga Wazazi walioleta kalamu wamefika

**Kiabatanisho II: Hojaji**

**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

Hojaji hii ni kwa ajili ya utafiti unaochunguza sintaksia ya kishazi tegemezi cha kisukuma mtazamo wa X-baa.

Tafadhali jibu maswali haya kwa mujibu uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yanayochangia maendeleo y kiswahili.Majibu ya maswali haya yatakuwa siri baina ya mtafiti na mtafitiwa.Weka tiki/vema mahali panapohusika.

i] Umri 15-24 [ ] 25-34 [ ] 35 -75 [ ]

ii] Jinsia Ke [ ] ME [ ]

iii] Kazi mwanafunzi, [ ] mwalimu [ ] mwanakijiji/mzee [ ]

1. Je, umewahi kuchanganua kishazi tegemezi? a) Ndiyo [ ] b) Hapana [ ]

2. Kama jibu ni hapana eleza maneno yanayovumishwa na kishazi tegemezi.

é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

é é é é é é é é é é é é é é é é é é

3. Je, kuna aina moja tu ya kishazi tegemezi kinachovumisha nomino au kiwakilishi tu?

a) Ndiyo [ ] b) Hapana [ ]

4. Je unawezaje kutambua kishazi tegemezi?

.....................................................................................................................................

.....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

5. .kishazi tegemezi kinaweza kuchanganuliwa kikamilifu kwa kutumia nadharia ya X-Baa.

a) ndiyo [ ] b) Hapana [ ]

**6.** Je, viambishi vipatanishi, njeo, na shamirisho vinaweza kuwa miundo virai kamili kwa kutumia nadharia ya X-Baa.? A) Ndiyo [ ] b) Hapana [ ]

Ahsante sana kwa ushirikiano wako

**Kiambatanisho Namba III: Dodoso**

**MASWALI YA MAHOJIANO**

1. Je, vishazi tegemezi vya kisukuma vina muundo gani ?

2). Je, umewahi kuchanganua kishazi tegemezi?

3). Ni vigezo gani vinavitumia kutambua kishazi tegemezi? Kutokana na vigezo hivyo kuna aina ngapi za vishazi tegemezi?

4. Je, kishazi tegemezi kinaweza kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia ya x-Baa?

5..Je, viambishi vipatanishi,njeo,na shamirisho vinaweza kuwa miundo kamili kwa kutumia nadharia ya X-Baa?

6.Je nadharia ya x-baa inafaa kuchanganulia kishazi tegemezi cha lugha ya kisukuma?